

**HALMASHAURI YA WILAYA KARAGWE.**  
**MUHTASARI WA KIKAO CHA BARAZA LA MADIWANI KILICHOFANYIKA KWENYE**  
**UKUMBI WA MIKUTANO WA KITUO RAFIKI CHA VIJANA (ANGAZA)**  
**TAREHE 03-04/05/2017.**

**WALIOHUDHURIA.**  
**WAJUMBE.**

<b>S/N.</b>	<b>JINA KAMILI</b>	<b>KATA</b>	<b>CHEO</b>
1.	Mh. Wallace Mashanda	Nyaishozi	<b>Mwenyekiti</b>
2.	Mh. Dawson .P. Byamanyirwohi	Rugera	Mjumbe
3.	Mh. Jovitha Kombe	V/M Nyabiyonza	Mjumbe
4	Mh. Fideli B. Mugabo	Bweranyange	Mjumbe
5.	Mh. Jane A. Bilaro	V/M Nyaishozi	Mjumbe
6.	Mh. Prisca .K. Busenene	V/M Kibondo	Mjumbe
7.	Mh. Genegeva J. Kanyiginya	V/M Kituntu	Mjumbe
8.	Mh. Magnus Kamugisha Cheusi	Kibondo	Mjumbe
9.	Mh. Zidina T. Murushid	Kituntu	Mjumbe
10.	Mh. Charles B. Beichumila	Nyakahanga	Mjumbe
11.	Mh. Joyce M. Aenda	V/M Kayanga	Mjumbe
12.	Mh. Justin T. Fidelis	Nyakabanga	Mjumbe
13.	Mh. Evalista Sylivesta	Kiruruma	Mjumbe
14.	Mh. Josephat B. Kinyina	Nyabiyonza	Mjumbe
15.	Mh. Adrian R. Kobushoke	Rugu	Mjumbe
16.	Mh. Edward E. Mpaka	Ndama	Mjumbe
17.	Mh. Wilbard R. Abdallah	Igurwa	Mjumbe
18.	Mh. Vaileth J. Kakuba	V/M Nyabiyonza	Mjumbe
19.	Mh. Mzakiru Mussa	Kamagambo	Mjumbe
20.	Mh. Leonard K. Ruhuna	Chanika	Mjumbe
21.	Mh. Felix R. Mkuchu	Ihembe	Mjumbe
22.	Mh. Xavery F. Buguzi	Nyakakika	Mjumbe
23.	Mh. Adventina C. Kahatano	Kayanga	Mjumbe
24.	Mh. Rwamuhangi S. Mugasha	Kayanga	Mjumbe
25.	Mh. Aneth K. Bagonza	V/M Kihanga	Mjumbe
26.	Mh. Novart Kishenyi	Chonyonyo	Mjumbe
27.	Mh. Vallace R. Kasumuni	Nyakasimbi	Mjumbe
28.	Mh. Aristides. B. Muliro	Bugene	Mjumbe
29.	Mh. Joackim January	Ihanda	Mjumbe
30	Mh. Sabby Rwazo	Kanoni	Mjumbe
31	Ndg. Eng. Wolta Kirita	Kaimu Mkurugenzi Mtendaji	<b>Katibu</b>

**WASIOHUDHURIA- KWA TAARIFA**

1	Mh. Innocent L. Bashungwa	Mbunge-Karagwe	Mjumbe
---	---------------------------	----------------	--------

**WATAALAM.**

S/N	JINA KAMILI	WADHIFA
1.	Ndg. Kiwango R. A.	Kaimu, Mkuu wa Idara ya Mipango, Takwimu na Ufuatiliaji
2	Ndg. Jackson Mwakisu	Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala
3	Ndg. Paschal Thomas	Mkuu wa Chuo KDVTC
4	Ndg. Beatus Nyarugenda	Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi
5	Ndg. Adeodatha Peter	Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Ustawi wa Jamii
6.	Ndg. Ashura Kajuna	Mkuu wa Kitengo cha Uchaguzi
7.	Ndg. Remigius Christian	Kaimu Mkuu wa Idara ya Mifugo na Uvuvi
8.	Ndg. Adam Salum	Kaimu Mkuu wa Idara ya Kilimo, Umwagiliaji na Ushiirika
9.	Ndg. Benson Abel	Kaimu Mkuu wa Idara ya Ardhi na Maliasili
10.	Ndg. Yudes .Z. Andrew	Mdhibiti Uboru wa Shule
11	Ndg. P. R. Rweyendera	Mkuu wa Idara ya Mazingira na usimamizi wa taka ngumu
12.	Ndg. Liberatus Rwazo	Kaimu Mkuu wa Idara ya Ujenzi
13	Ndg. Edius Rwangoga	Mratibu TASAF
14.	Ndg. Rajab Khasimu	Mkuu wa Kitengo cha Ufugaji Nyuki
15.	Ndg. Sechelela Kallim	Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari
16	Ndg. Mhela F. Lufungulo	Katibu TSC (W)
17.	Ndg. Donati Bunonosi	Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi
18	Ndg. Hernam Kigwa	Mkuu wa Idara ya Maji
19	Ndg. Medani Jekamaya	Mhasibu
20	Ndg. Edward Malima	Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara
21	Ndg. Rogath Timanywa	Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Manunuzi na Ugavi
22	Ndg. Peter K. Evarister	Afisa Biashara
23	Dr. Libamba Sobo	Mkuu wa Idara ya Afya
24	Ndg. Dickson Sabe	Mkuu wa Kitengo cha Ukaguzi
25	Ndg. Devotha Tibanywana	Kaimu Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji mdogo wa Kayanga
26	Ndg. Wilking Shuma	Meneja maji Mjini
27.	Ndg. Samwel Manumbu	Mchumi

**WAALIKWA.**

<b>S/N</b>	<b>JINA KAMILI</b>	<b>WADHIFA/ANAKOTOKA</b>
1.	Mhe. Godfrey Mheluka	Mhe. Mkuu wa Wilaya
2	SSP. M.S. Nasolwa	D.P.O
3.	Ndg. Innocent Nseni	Katibu tawala (W)
4.	A/Insp/ Faith Mbagwa	A/ISP/IMM
5.	Ndg. Peterson Mushenyera	Katibu NSSR-Mageuzi
6.	Ndg. Madanio Swalehe	Katibu CUF (W)
7.	Ndg. Ndibalema Kanyambo	Katibu-CHADEMA (W)
8	Ndg. Robinson Mutafungwa	M/Kiti CCM (W)
9	Ndg. Amri O. Mtabazi	Katibu CCM (W)
10.	Ndg. Amos P. Kahwa	Mamlaka ya Mji Mdogo Kayanga
11	Ndg. Revelian Policalipo	Mwakilishi TLP (W)
12.	Ndg. Benneth K. Ruhinda	Katibu UDP (W)
13.	Ndg. Linus Kishenyi	ACT Wazalendo (W)
14.	Ndg. Jovinus Ezekiel	Radio KARAGWE
15.	Ndg. Peter Mmbare	DFO
16.	Ndg. Rashida Mfaume	For. DCB
17.	Ndg. Ivo Ndisanye	Katibu wa Mbunge
18.	Ndg. Romanus Msafiri	DSO
19.	SSP. Mika Makanja	OCD – Karagwe
20	Ndg. Devotha Martin	Radio Fadeco
21	Ndg. Gregory Gabone	Mkiti CHADEMA
22	D/DIO-Feruzi Said	AIS
23	Cpt. S. K. Hango	MJA
24	Ndg. Ellen Magambo	Redio KWIZERA

**MAAFISA TARAFU**

<b>S/N</b>	<b>JINA KAMILI</b>	<b>TARAFU</b>
1.	Ndg. Erasto Haganja	Nyabiyonza
2.	Ndg. Medard Baletwa	Kaimu, A/Tarafa-Nyaishozi
3.	Ndg. Nyangele Makunenge	Kituntu
4	Ndg. Rozalia Njiani	Bugene
5.	Ndg. Gratian Kikabiha	Nyakakika

## **SEKRETARIETI.**

1. Geoffrey A. Kazaula
2. Joyce H. Kitundu

## **DONDOO**

### **TAREHE 03/05/2017**

1. Kufungua Kikao
2. Kuthibitisha Dondoo
3. Kupokea taarifa yoyote inayopaswa kupokelewa kwa mujibu wa sheria
  - (i) Taarifa ya Serikali
  - (ii) Taarifa ya Mwenyekiti
4. Kupokea na kujadili taarifa za Kata kutoka kwa Wenyeviti wa WDC.
5. Maswali ya papo kwa papo kutoka kwa Wajumbe wa Baraza la Madiwani.
6. Kuahirisha Kikao.

### **TAREHE 04/05/2017**

7. Kufungua Kikao
8. Kusoma na kuthibitisha Muhtasari wa kikao cha Baraza la Madiwani cha tarehe 21-22/2/2017.
9. Taarifa ya utekelezaji wa maazimio ya Kikao cha tarehe 21-22/2/2017.
10. Kupokea taarifa za utendaji na uwajibikaji wa Halmashauri kutoka kwa Wenyeviti wa Kamati za Kudumu.
  - i. Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango Kikao cha tarehe 28/02/2017, tarehe 24/03/2017 na tarehe 20/04/2017.
  - ii. Kamati ya Elimu, Afya na Maji kikao cha tarehe 18/04/2017.
  - iii. Kamati ya Uchumi, Ujenzi na Mazingira kikao cha tarehe 12/04/2017.
  - iv. Kamati ya Kudhibiti UKIMWI kikao cha tarehe 24/04/2017.
11. Taarifa za Mkurugenzi Mtendaji.
  - i. Taarifa ya Mapato na Matumizi kwa robo ya tatu, 2016/2017.
  - ii. Taarifa ya Manunuzi na Bodi ya Zabuni robo ya tatu, 2016/2017.
  - iii. Taarifa ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai-Machi 2016/2017.
  - iv. Taarifa ya mikopo ya Vikundi vya Wanawake na Vijana kwa robo ya tatu, 2016/2017.
  - v. Taarifa ya vikao vya kisheria vilivyofanyika ngazi ya Kata na Vijiji kwa robo ya tatu 2016/2017.
  - vi. Taarifa ya Ukaguzi wa Ndani kwa kipindi cha robo ya tatu, 2016/2017.
  - vii. Taarifa ya madeni ya ujenzi wa vyumba vya maabara Shule za Sekondari.

- viii. Mapendekezo ya kurekebisha sheria ndogo na 01 vipengele 1-9 ya mwaka 2011, juu ya kodi za usombaji wa madini ya ujenzi.
- ix. Masuala ya kiutumishi.

12. Kufunga Kikao.

### **KUMB. NA. 90/2016/2017/8 - KUFUNGUA KIKAO**

Akifungua kikao Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao cha kawaida cha robo ya tatu ili kujadili taarifa zilizowasilishwa.

Aliwapongeza Menejimenti na Waheshimiwa Madiwani kwa utekelezaji wa shughuli zote za kusimamia maendeleo na ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha robo ya tatu kwa ufanisi. Aidha aliipongeza Serikali kwa utekelezaji wa masuala muhimu likiwemo suala la uhamishaji wa mifugo katika pori la Kimisi.

Alieleza kuwa hadi sasa Halmashauri imekusanya asilimia 51.17, hivyo alitoa msisitizo kuwa Halmashauri iendeleo kukusanya mapato yake kikamilifu ili kufikia malengo ya kukusanya asilimia 80.

Aliipongeza Serikali Kuu kwa ajili ya kutoa zaidi ya TSh. Bilioni moja kwa lengo la utekelezaji wa Miradi ya maji kwa Miji ya Kayanga na Bugene chini ya BUWASA. Aidha kuhusu fedha zilizokuja za Miradi sita ya Maji alisisitiza kuwa utekelezaji wa Miradi hiyo ufanyike kwa haraka ili kukidhi tarehe ya mwisho ya utekelezaji na kuanza mkakati wa utekelezaji wa miradi mingine kwa Vijiji vingine kumi.

Alitoa taarifa kuwa Serikali italeta fedha kwa ajili ya kununua madawa na vifaa tiba. Aidha kwa sasa Zahanati na Vituo vya Afya vina dawa za kutosha. Kuhusu Zahanati na Vituo vya Afya ambavyo havijasajiliwa na kwamba usajili wake unategemea ruhusa kwa ngazi ya Mkoa ili kutuma maombi ya usajili huo Wizara husika, alitoa wito kuwa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya asaidie kushauri ngazi ya Mkoa kuruhusu usajili huo ili wananchi waanze kupata huduma.

Kikao kilifunguliwa mnamo saa 3:52 asubuhi.

### **KUMB. NA. 91/2016/2017/8 - KUTHIBITISHA DONDOO.**

Wajumbe walijadili taarifa zilizowasilishwa na kuongeza taarifa moja ambayo ni taarifa ya Mapendekezo ya Wajumbe wa Baraza la Kata Bweranyange.

Baada ya nyongeza hiyo wajumbe walikubaliana kuwa Dondoo hizo ndizo zijadiliwe.

**KUMB. NA. 92/2016/2017/8 - KUPOKEA TAARIFA YOYOTE INAYOPASWA KUPOKELEWA KWA MUJIBU WA SHERIA.**

**i. TAARIFA YA SERIKALI (TAARIFA YA DC).**

Akitoa taarifa ya Serikali Mkuu wa Wilaya aliwapongeza Madiwani kwa kushirikiana na Menejimenti kwa utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Alisisitiza kuwa ataendelea kufuatilia kwa karibu ufunguzi wa Zahanati zilizokamilika kwa kushirikiana na Ofisi ya Katibu Tawala wa Mkoa. Alieleza kuwa Kamati ya Ulinzi na Usalama imefanya zoezi la kuondoa mifugo ndani ya pori la Kimisi na kueleza kuwa katika utekelezaji wa zoezi hilo mifugo yote inayomilikiwa na wananchi wa Karagwe ilifanikiwa kurudishwa kwa wamiliki wake. Kuhusu kampeni dhidi ya madawa ya kulevya aliomba ushirikiano kwa Waheshimiwa Madiwani na wananchi kwa ujumla kuhakikisha wanatoa taarifa kwa wakati pale wanapobaini uwepo wa madawa ya kulevya na viroba katika maeneo yao.

Kuhusu ukaguzi wa vyeti kwa watumishi alieleza kuwa jumla ya watumishi 52 wamebainika katika Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe wakiwa na vyeti bandia na alisisitiza kuwa watumishi hao waondoke ofisini kama ilivyoagizwa na Serikali.

Kuhusu suala la wahamiaji haramu alisisitiza kuwa wananchi wasiwapokee wahamiaji haramu na kwamba watakaobainika kufanya hivyo watachukuliwa hatua za kisheria ikiwa ni pamoja na makazi yao kutaifishwa.

Baada ya hotuba ya Mkuu wa Wilaya wajumbe walipata nafasi ya kuchangia kama ifuatavyo;

Mjumbe alipongeza kazi iliyofanywa na Kamati ya Ulinzi na Usalama na kuiomba Kamati hiyo kuendelea kushughulikia suala la uhamiaji holela wa ndani kwa ndani.

Mjumbe mwingine alimuomba Mhe. Mkuu wa Wilaya na Kamati ya Ulinzi na Usalama kushughulikia suala la uvuvi haramu katika maeneo mbali mbali.

Kuhusu operesheni ya kuondoa wahamiaji haramu katika maeneo mbali mbali, ilifafanuliwa kuwa tayari watendaji wa Kata wamepewa maelekezo na kwamba zoezi hilo litafanyika baada ya wananchi kuvuna mazao yao.

**ii. TAARIFA YA MWENYEKITI.**

Mwenyekiti alimkaribisha mtaalam kutoka Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ili kutoa elimu juu ya kupambana na Rushwa.

Akitoa Elimu juu ya kupambana na rushwa alisisitiza kuwa utekelezaji wa miradi mbali mbali ya maendeleo unapaswa kuzingatia thamani ya pesa. Alieleza pia kwamba Wah.

Madiwani wana wajibu wa kusimamia miradi ya maendeleo ikiwa ni pamoja na kuhakikisha miradi yote inatekelezwa kwa uwazi.

Aliwatahadharisha viongozi mbali mbali kuzingatia sheria wakati wa utekelezaji wa majukumu yao huku akieleza kuwa bado kuna malalamiko mengi kutoka kwa wananchi dhidi ya viongozi wanaokiuka sheria na kupokea rushwa.

### **KUMB. NA. 93/2016/2017/8 - KUPOKEA NA KUJADILI TAARIFA ZA KATA KUTOKA KWA WENYEVITI WA WDC.**

Wenyeviti wa Kamati za Maendeleo ya Kata waliwasilisha taarifa za Kata kama zilivyopitishwa na WDC zao.

Taarifa zilizowasilishwa ni zile zinazojadiliwa kwenye WDC zinazohusiana na vikao vya kisheria kwa robo husika, Miradi ya maendeleo kwenye Kata, mapato na matumizi na changamoto zinazokuwa zimejitokeza kwenye Kata.

#### **Kata zifuatazo ziliwasilisha taarifa:**

1. Kata ya Nyakahanga
2. Kata ya Kamagambo
3. Kata ya Igurwa
4. Kata ya Bugene
5. Kata ya Rugu
6. Kata ya Ndama
7. Kata ya Chonyonyo
8. Kata ya Kihanga
9. Kata ya Nyakasimbi
10. Kata ya Nyabiyonza
11. Kata ya Chanika
12. Kata ya Nyakabanga
13. Kata ya Kayanga
14. Kata ya Nyakakika
15. Kata ya Ihembe
16. Kata ya Kanoni
17. Kata ya Kibondo
18. Kata ya Kituntu
19. Kata ya Nyaishozi
20. Kata ya Kiruruma
21. Kata ya Rugera
22. Kata ya Bweranyange

Kwa upande wa Kata ya Ihanda Mhe. Diwani hakuwasilisha taarifa kwa madai kwamba taarifa iliyoletwa na Mtendaji wa Kata hiyo si sahihi.

Wakijadili taarifa za Kata wajumbe walishauri kwamba taarifa ya Kata ya Ihanda ifanyiwe mapitio na Ofisi ya Mkurugenzi pamoja na Mwenyekiti ili kujiridhisha na utata huo ulioibuliwa na Mhe. Diwani.

Aidha wajumbe walisisitiza kuwa Halmashauri inapaswa kuwezesha Kata na Vijiji ili ziweze kutimiza majukumu yake ipasavyo, huku wakieleza kuwa taarifa nyingi zilizowasilishwa zilikosa usahihi katika takwimu.

Wajumbe walisisitiza kuwa mfumo wa uandaaji wa taarifa za Kata utumike katika kuandaa taarifa za Kata za robo. Aidha wajumbe walishauri kuwa fedha za Elimu Bure zisimamiwe vizuri kwa kuhakikisha kifungu cha ukarabati kinatumika vizuri kama ilivyopangwa.

Wajumbe walilalamikia upungufu wa watumishi katika ngazi za chini. Ilifafanuliwa kuwa jambo hilo litafanyiwa kazi baada ya kibali cha ajira kutoka.

Kuhusu usahihi wa taarifa na takwimu mbali mbali wajumbe **waliazimia** kuwa Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala awaelekeze Watendaji wa Kata namna ya kuandaa takwimu sahihi na kutoa taarifa zenye uhalisia.

Wajumbe waliongeza kuwa Wenyeviti wa WDC ambao ni Wah. Madiwani wana wajibu wa kusimamia taarifa zinazotolewa na Watendaji wa Kata na kujiridhisha kuwa ni sahihi.

Kuhusu ufanyikaji wa vikao vya Kamati za Maendeleo za Kata wajumbe walisisitiza kuwa vikao hivyo viwe vinafanyika kwa wakati, na kueleza kuwa kwa Kata zilizoko Mamlaka ya Mji Mdogo vikao vyao viwe vinafanyika tarehe 08, na Kata nyinginezo zifanye vikao hivyo kati ya tarehe 15 na 16 ili kuhakikisha ifikapo tarehe 25 Kata ziwe zimefanya vikao hivyo.

Kuhusu ufanyikaji wa vikao mbali mbali wajumbe **waliazimia** kuwa kila taarifa inayowasilishwa kuanzia ngazi ya Kitongoji, Kijiji hadi WDC iambatane na Muhtasari ili kuonesha usahihi wa taarifa hiyo na kwamba muhtasari wa Kamati ya kudhibiti UKIMWI pia uwasilishwe sambamba na taarifa hiyo.

**KUMB. NA. 93/2016/2017/8 - MASWALI YA PAPO KWA PAPO KUTOKA KWA WAJUMBE WA BARAZA LA MADIWANI.**



1. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Adrian Kobushoke wa Kata ya Rugu**, yeye alitaka kujua mpango wa Halmashauri kuwapatia eneo Shirika la Nyumba la Taifa ili kujenga nyumba badala ya kuchukua nyumba za watumishi zinazotumika kwa sasa. Ilijibiwa kwamba Halmashauri kwa sasa haina eneo na kwamba nyumba hizo zitajengwa na TBA katika eneo hilo la NHC la sasa na kwamba baada ya ujenzi litatolewa ombi maalum kuwapa kipaumbele watumishi wanaotumia nyumba hizo kwa wakati huu.
2. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Jovitha Kombe wa Viti Maalum Nyabiyonza**, yeye alitaka kujua eneo ambalo Halmashauri ina mpango wa kujenga Hospitali ya Wilaya. Ilijibiwa kuwa ufuatiliaji wa kuomba eneo hilo unaendelea ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya athari za kimazingira kwa kushirikiana na Idara ya Ardhi.
3. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Valence Kasumuni wa Kata ya Nyakasimbi**, yeye alitaka kujua mpango wa Halmashauri wa kuweka watu wa kufanya usafi katika maeneo ya masoko, magulio na minada. Ilijibiwa kuwa uongozi wa Kata ukae na kuweka utaratibu wa ufanyakaji wa usafi katika maeneo hayo.
4. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Magnus Cheusi wa Kata ya Kibondo**, yeye alitaka kujua ni mpango gani uliopo katika kuajiri Watendaji wa Kata na Vijiji. Ilijibiwa kwamba jamno hilo linasubiri vibali vya ajira kutoka Serikalini kama ilivyofafanuliwa na Mkurugenzi Mtendaji.
5. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Rwamuhangi Mugasha wa Kata ya Kihanga**, yeye alitaka kujua juu ya fedha za Mradi wa Maji wa Kakiki na kwamba lini utakarabatiwa. Ilijibiwa kuwa mradi huo unatarajia kutumia fedha za CDG na kwamba pindi zikiletwa ukarabati utafanyika.
6. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Wilbard Abdallah wa Kata ya Igurwa**, yeye alitaka kujua mpango wa Halmashauri kukarabati Ofisi ya Kata baada ya kuathiriwa na tetemeko. Ilifafanuliwa kuwa mfuko wa maafa tayari ulifungwa, hivyo Mhe. Diwani afanye uhamasishaji kwa wadau mbali mbali ili kufanya ukarabati huo.
7. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Leonard Ruhuna wa Kata ya Chanika**, yeye alitaka kujua ni lini Waheshimiwa Madiwani watapewa Ilani ya Uchaguzi ili kurahisisha utekelezaji wao. Ilijibiwa kuwa Ilani hiyo watapewa.
8. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Evarister Sylvester wa Kata ya Kiruruma**, yeye alitaka kujua juu ya mkakati wa ukusanyaji wa ushuru wa minara ya simu kwa

makampuni mbali mbali. Ilijibiwa kuwa suala la ukusanyaji wa minara litafafanuliwa kwenye taarifa za Kamati.

9. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Novath Kishenyi wa Kata ya Chonyonyo**, yeye alitaka kujua juu ya uwekaji wa minyororo kwenye stendi ya Omurushaka ili kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Halmashauri. Ilifafanuliwa kuwa jambo hilo litafanyika baada ya kubadili sheria ndogo ya Mamlaka ya Mji Mdogo.
10. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Adventina Kahatano wa Kata ya Kayanga**, yeye alitaka kujua juu ya mpango wa kuandika maandiko mbali mbali ya kuomba fedha kwa Wahisani. Ilijibiwa kwamba Wahisani wengi wanapenda kufanya kazi na kutoa fedha kwa NGO's moja kwa moja na sio kwa Halmashauri.
11. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Edward Mpaka wa Kata ya Ndama**, yeye alitaka kujua ni kwanini mifugo iliyotolewa katika pori la Kimisi haikutozwa ushuru. Ilifafanuliwa kuwa hilo lilikuwa ni agizo la Serikali ili kufanikisha utekelezaji wa agizo hilo.
12. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Josephat Kinyina wa Kata ya Nyabiyonza**, yeye alitaka kujua mpango wa Halmashauri wa kuchanja mifugo kwani mifugo iliyotoka porini ilikuwa na magonjwa. Ilijibiwa kwamba hatua ya kwanza itawekwa karantini baada ya mifugo kuwa wamethibitika kuugua.
13. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Justin Fidelis wa Kata ya Nyakabanga**, yeye alitaka kujua mpango wa Halmashauri kusaaidia Kamati za Shule kukusanya fedha za michango ya chakula na utunzaji wa fedha hizo. Ilijibiwa kuwa Maafisa Elimu walifanyie kazi suala hilo na kuhakikisha fedha zinakusanywa kwa risiti na kwa utaratibu maalum. Baraza la Madiwani lilieleza kuwa utaratibu huo wa ukusanyaji fedha kiholela lisitishwe mara moja na Wakuu wa Shule waelekezwe kuzingatia Waraka wa Elimu Bure.
14. **Swali kutoka kwa Mhe. Diwani Mzakiru Musa wa Kata ya Kamagambo**, yeye alitaka kujua hatua za ufunguzi wa Shule ya Kilegete. Ilijibiwa kuwa wadhhibiti Ubora wa Shule watatoa taarifa za ukaguzi wa shule hiyo Wizarani ndipo hatua nyingine zitafuata.

**SIKU YA PILI TAREHE 04/05/2017.**

**KUMB. NA. 94/2016/2017/8 - KUFUNGUA KIKAO.**

Mwenyekiti alifungua Kikao mnamo saa 3:39 Asubuhi.

**KUMB. NA. 95/2016/2017/8 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 22-23/11/2016.**

Wajumbe waliusoma muhtasari na kufanya masahihisho yafuatayo;  
Uk 1 jina na 25 'kata ya Kayanga' lisomeke 'Kata ya Kihanga'  
Uk 6 jina na 28 'Vallace' lisomeke 'Vallence'  
Uk 10 neno 'kibishara' lisomeke 'kibiashara'  
Uk 46 neno 'hazijasambazwa' lisomeke 'hazijasambazwa'  
Uk 48 kipengele 10.2 kifutwe chote.

Baada ya masahihisho hayo muhtasari ulisainiwa na Mwenyekiti kuwa kumbukumbu sahihi za kikao.

**KUMB. NA. 96/2016/2017/8 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 21-22/02/2017.**

**Hoja na 1-** Baada ya uwasilishwaji na utambulisho wa Kampuni ya NAMAIGO, wajumbe waliazimia kuwa Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Idara nyinginezo kulingana na aina ya mradi husika iratibu kampuni mbali mbali zinazojitokeza kufanya kazi na wananchi, ikiwa ni pamoja na kuzitambulisha kampuni hizo kwa wananchi ili ziweze kufanya kazi na jamii husika.

**Utekelezaji-** Azimio limezingatiwa, ushirikiano utaendelea kutolewa kwa makampuni na mashirika yatakayojitokeza.

**Hoja na 2 -** Kuhusu mkanganyiko wa ulipaji nauli uliopo kwa wananchi, wajumbe waliazimia kuwa Afisa Biashara pamoja na Mhandisi wa Ujenzi wapime na kubaini urefu uliopo kutoka Makao Makuu ya Wilaya hadi Vituo vyote vya biashara kisha wawapatie SUMATRA umbali huo ili uwasaidie katika kutoa elimu kwa wananchi juu ya viwango vya nauli vinavyopaswa kulipwa.

**Utekelezaji-** Azimio limetekelezwa kwa barua yenye Kumb. Na. KGR/HWK/41/1/40 kwenda SUMATRA Bukoba.

Wakijidili hoja hiyo wajumbe walieleza kuwa hoja hiyo haikutekelezwa kikamilifu na kuagiza kuwa suala hilo lifanyiwe utekelezaji kikamilifu.

**Hoja na 3-** Wakijadili taarifa za WDC, wajumbe waliagiza kuwa wakati wa uandaaji wa taarifa hizo mambo yafuatayo yazingatiwe.

Taarifa ya mapato na matumizi katika vijiji, kata, shule na zahanati, hali ya upatikanaji wa dawa katika zahanati na vituo vya afya, mwenendo wa mfuko wa CHF, upatikanaji wa uji na chakula shuleni, mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji, taarifa ya vifo vya akina mama na watoto,

taarifa ya vikao vya kisheria, taarifa ya utoro shuleni, udhibiti wa utoro na maendeleo ya taaluma, ufanyikaji wa vikao vya kamati ya kudhibiti UKIMWI ngazi ya kata.

**Utekelezaji-** Azimio limezingatiwa. Fomati mpya imeandaliwa inayojumuisha mambo yote muhimu kama ilivyoelekezwa na Baraza na imetumwa kwa Watendaji wote wa Kata na Vijiji.

**Hoja na 4-** Kuhusu usimamizi wa Elimu, wajumbe **waliazimia** kuwa Waratibu wa Elimu Kata wasimamiwe ili kuhakikisha wanatimiza wajibu wao wa kusimamia elimu katika kata.

**Utekelezaji-** Ushauri umezingatiwa, Maafisa Elimu Kata wanaendelea kusimamiwa katika kutekeleza majukumu yao ya kusimamia elimu katika Kata.

**Hoja na 5-** Kuhusu usimamizi wa mazingira na vyanzo vya maji, wajumbe **waliazimia** kuwa Idara ya Mazingira na Usimamizi wa taka ngumu isimamie na kuhakikisha miti yote iliyopandwa inalindwa na kukua.

**Utekelezaji-** Azimio limezingatiwa, uhamasishaji na usimamizi utaendelea kufanyika hasa kipindi hiki cha mvua.

**Hoja na 6-** Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa kuhusu eneo hilo linalopendekezwa kujengwa Hospitali ya Wilaya, taratibu za kuiomba sehemu inayo milikiwa na wakala wa Barabara – TANROADS zifanyike haraka ili eneo hilo liweze kumilikiwa na Halmashauri, kupatiwa hati na kikao kijacho taarifa kamili itolewe.

**Utekelezaji-** Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji iliandika barua juu ya maombi ya eneo husika kwa TANROADS Mkoa na barua hiyo iliandikwa mnamo tarehe 25/11/2016 yenye Kumb Na KGR/HWK/9.7/2B/1/2/ na kujibiwa kwa barua yenye Kumb Na KGR/TANR/108/242/Vol IV/17 ya tarehe 25/11/2017 iliyoagiza kumwandikia barua Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi . Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji imekwisha mwandikia barua Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi ya tarehe 1/03/2017 yenye Kumb. Na. KGR/HWK/T.7/2B/1/109.

Wakiijadili hoja hiyo, wajumbe walishauri kwamba Timu ya Wataalam wafike eneo husika na watoe majibu sahihi ya kitaalam ikiwa ni pamoja na athari za kimazingira.

**Hoja na 7-** Kuhusu Zahanati mbali mbali zilizofikia hatua ya ukamilikaji, hatua za kukamilisha Zahanati hizo zichukuliwe haraka ili ziweze kufunguliwa na kutoa huduma kwa wananchi, kikao kijacho taarifa itolewe.

**Utekelezaji-**Taarifa ilitolewa kwenye kikao.

**Hoja na 8-** Kuhusu ushuru wa maegesho, wajumbe waliazimia kuwa maeneo ya magari kupaki yaainishwe, Mnyororo uwekwe katika stendi ya Omurushaka kwa kuelekeza magari kuingia na kutoka ndani ya stendi ili yaweze kulipia ushuru.

**Utekelezaji-** Kazi inaendelea.

**Hoja na 9-** Watendaji wa Kata ambao Kata zao zinapakana na minada, waandikiwe barua na kuelekezwa kuwa siku ya mnada wahakikishe wanasimamia ukusanyaji wa ushuru wa mifugo kwa kushirikiana na Maafisa Tarafa na kuhakikisha mifugo yote inalipiwa bila kutoroshwa.

**Utekelezaji-** Azimio limezingatiwa na Watendaji wote wameandikiwa barua yenye kumb. Na. KGR/HWK/T4/34/VOL.V/56 ya tarehe 01/03/2017 ya kuwataka kusimamia ukusanyaji wa mapato/ushuru wa mifugo katika Kata zao.

**Hoja na 10-** Kuhusu maeneo ambapo kahawa zilinyauka pamoja na migomba kutokana na jua kali lililowaka kwa kipindi kirefu, wajumbe **waliazimia** kuwa Mabwanashamba waagizwe kuwashauri wananchi namna ya kukata kahawa hizo ili zichipue upya pamoja na migomba, aidha waagizwe kuwaelekeza wananchi kutengeneza makinga maji na kuelekeza maji ya mvua katika mashamba yao.

**Utekelezaji-** Maafisa Ugani wote walihimizwa kwa kuandikiwa barua yenye Kumb. Na. KGR/HWK/T.15/4/VOL.V ya tarehe 03/03/2017. Barua hii iliwaagiza kuwahimiza wakulima wakate matawi ya kahawa na migomba yaliyokauka na kuelekeza maji ya mvua mashambani kwa kutengeneza makinga maji. Barua hiyo iliwataka Watendaji wa Kata na Vijiji kusimamia zoezi hilo. Aidha kwenye kikao cha tarehe 24/04/2017 Maafisa Ugani wote wamekumbushwa suala hilo.

Wakiijadili hoja hiyo mjumbe alitaka kujua ni kwanini miche ya kahawa haikugawiwa kwa wananchi. Ilifafanuliwa kuwa miche hiyo iligawiwa lakini mingi ilikauka kutokana na ukame wa muda mrefu. Ilitolewa taarifa pia kuna vikundi vya wanachi ambavyo vinazalisha mbegu kwa hivyo wananchi watajulishwa ili kununua miche hiyo kwa bei nafuu kutoka kwa vikundi hivyo. Aidha kuna shirika la OLUM ambalo watauzi miche hiyo kwa wanachi kwa bei nafuu msimu wa mvua utakapofika.

Wajumbe walishauri kuwa Maafisa Ugani na wataalam watoe maelekezo na elimu kwa viongozi wote wa ngazi za chini na wafike mashambani kuwaelimisha wananchi juu ya kutoa machipukizi katika mashamba yao, kuandaa mashamba kwa kuchimba mashimo ya kupanda miche na kuweka mbolea mapema kabla ya msimu wa mvua.

Aidha walisisitiza kuwa takwimu na majina ya wakulima waliojiandaa yawasilishwe Idara ya Kilimo kufikia mwisho wa mwezi wa nane.

**Hoja na 11-** Kuhusu mgogoro wa mipaka katika Kata za Nyakabanga na Nyakasimbi, wajumbe **waliazimia** kuwa Idara ya Ardhi na Maliasili iendelee kulifanyia kazi suala hilo na kutoa taarifa kamili kikao kijacho kwa kuhakikisha mkanganyiko huo unakwisha.

**Utekelezaji-** Utekelezaji utafanyika baada ya kupata COMPAS BEARING ambayo inayotarajia kuazimwa toka Ofisi ya RAS Kagera kwani Halmashauri haina kifaa hicho.

Wakijadili taarifa hiyo wajumbe walieleza kuwa utekelezaji wa agizo hilo hauridhishi na **kuazimia** kuwa agizo hilo litekelezwe upya na kwamba ifikapo tarehe 4/6/2017 itolewe taarifa juu ya upatikanaji wa kifaa hicho ili kumaliza mgogoro huo wa mipaka ya Kata za Nyakasimbi na Nyakabanga. Taarifa hiyo itolewe kwa Mkurugenzi Mtendaji na nakala kwa Mwenyekiti.

Wajumbe walishauri pia kuwa Idara ya Ardhi na Maliasili isimamiwe kikamilifu ili kutekeleza shughuli zake kwa umakini. Aidha vijiji vyote vyenye migogoro viletwe rasmi kwa maandishi ili kupata suluhu za migogoro hiyo.

## **KUMB. NA. 97/2016/2017/8 - KUPOKEA TAARIFA ZA UTENDAJI NA UWAJIBIKAJI WA HALMASHAURI KUTOKA KWA WENYEVITI WA KAMATI ZA KUDUMU.**

### **TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO.**

Ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kutokana na kikao kilichoketi tarehe 28/02/2017 kuanzia saa 4:22 asubuhi . Kikao kilichohudhuriwa na wajumbe 10 kati ya kumi na wataalam waliohudhuria walikuwa ni 27.

Kikao kilizingatia agenda kama inavyooneshwa kwenye Dondoo zifuatazo:

#### **1.0 KUMB. NA. 89/2016/2017/8 - KUFUNGUA KIKAO.**

- 1.1 Akifungua kikao, Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao cha kawaida na alisisitiza kuwa maazimio ya kikao cha Baraza la Madiwani yafanyiwe kazi kwa wakati.
- 1.2 Aidha, alisisitiza kuwa Menejimenti ifuatilie kwa karibu vyanzo vya mapato na hasa minada ya Nyaishozi na Rukole.
- 1.3 Kuhusu sheria ndogo, Mwenyekiti alisisitiza kuwa sheria hizo zifuatiliwe haraka ili ziweze kukamilika na hatimaye kutumika katika kukusanya mapato.
- 1.4 Kikao kilifunguliwa mnamo saa 4: 22 Asubuhi.

#### **2.0 KUMB. NA. 90/2016/2017/8 - KUTHIBITISHA DONDOO.**

- 2.1 Wajumbe walijadili Dondoo zilizowasilishwa na kuongeza dondoo zifuatazo:-
  1. Kuomba kibali cha matumizi ya TSh. 64,157,330.00 kutoka katika vifungu vya matumizi ya Mradi wa MDH chini ya Sekta ya Idara ya Afya.

2. Mapendekezo ya kutoa mikopo kwa Vikundi vya Wanawake na Vijana kwa kipindi cha Januari - Machi, 2017.
- 2.2 Baada ya kuongeza dondoo hizo, wajumbe walikubaliana kuwa dondoo hizo ndizo zijadiliwe.

**3.0 KUMB. NA. 91/2016/2017/8 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 27/1/2017.**

- 3.1 Wajumbe walisoma muhtasari na kufanya masahihisho yafuatayo:-
- 3.2 Uk 3 neno 'kuwa' lisomeke - kuwahi
- 3.3 Neno 'kilifunguliwa' lisomeke - kilifunguliwa
- 3.4 Uk 6 - neno 'Disemba' lisomeke - Desemba.
- 3.5 Baada ya kufanya masahihisho hayo, wajumbe walikubaliana kuwa muhtasari huo uwe kumbukumbu sahihi za vikao na kisha ulisainiwa na Mwenyekiti.

**4.0 KUMB. NA. 92/2016/2017/8- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 27/01/2017.**

- 4.1 Hoja Na. 1 kuwa Watendaji wa Kata waandikiwe barua kuwataka watambue minara yote iliyopo katika maeneo yao, na waainishe minara hiyo ipo kwenye ardhi inayomilikiwa na nani. Aidha, minara yote ya simu ipelekewe hati ya madai "**Demand note**" ya **TSh. 60,000,000/=** kwa kila mnara.
- 4.2 **Utekelezaji** - Minara ipo 33 na kati ya hiyo, minara 2 tu ipo kwenye maeneo ya Taasisi za Serikali ambazo ni Shule ya Msingi Rugu na Shule ya Msingi Kayanga.
- 4.3 Wajumbe **waliagiza** kuwa ufuatiliaji juu ya suala hilo uendeleo kufanyika, Watendaji wa Kata na Vijiji wabaini minara yote iliyopo katika maeneo yao na washirikishe viongozi wenzao katika vikao vya WDC na Serikali za Vijiji kisha iandaliwe taarifa ya maandishi kwa kila eneo ambayo itaonesha ni lini minara hiyo imeanza kufanya kazi, ni ya kampuni gani na iko kwenye ardhi ya nani.
- 4.4 Baada ya kupatikana kwa taarifa hiyo, wajumbe walishauri kuwa TAMISEMI waandikiwe barua kufahamishwa juu ya madai ya ushuru wa huduma ambao Halmashauri inadai kutoka kwa Makampuni ya Simu na kwamba barua hiyo apewe nakala Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.
- 4.5 **Hoja Na. 2** Mjumbe alitoa hoja juu ya ahadi ya wamiliki wa minara ya Halotel kuweka huduma ya "internet" Ofisi zote za Umma. Kikao **kiliazimia** kuwa Mikataba ya Kampuni hiyo ipitiwe upya ili kujiridhisha na jambo hilo.
- 4.6 **Utekelezaji** - Wajumbe walishauri kuwa ufuatiliaji uendeleo kama ilivyo katika agizo la kwanza.

- 4.7 **Hoja Na. 3** Mjumbe alitoa hoja kuwa baadhi ya Maafisa Mifugo wamekuwa wadanganyifu katika kuwasilisha mapato yanayotokana na ushuru na tozo mbali mbali zitokanazo na mifugo mfano Afisa Mifugo wa Kata ya Bugene na Kituntu.
- 4.8 Kikao **kiliazimia** kuwa Maafisa Mifugo waandikiwe barua kuwataka wafike ofisini na vitabu vyao vya makusanyo ili ukaguzi yakinifu ufanyike.
- 4.9 **Utekelezaji** - Ukaguzi yakinifu ulifanyika chini ya Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara.
- 4.10 Wajumbe walishauri kuwa vitabu vinapo pelekwa katika Kata husika, taarifa itolewe katika WDC na kwamba taarifa za kila robo mwaka za WDC zitaje pia vitabu vilivyopo katika Kata.
- 4.11 Aidha, wajumbe walishauri kuwa Kitengo cha Ukaguzi kifanye kazi katika maeneo yote kwa kuhakikisha ukaguzi unaendelea kufanyika hata ngazi za vijiji.
- 4.12 **Hoja Na. 4** Mjumbe alihoji juu ya ukusanyaji wa mapato yote kwa kutumia “POS” kama inafanyika hivyo kwa maeneo yote. Ilifafanuliwa kuwa kwa baadhi ya maeneo inafanyika hivyo. Aidha kwa sasa Halmashauri imetenga TSh. 10,000,000.00 kwa ajili ya kuongezea maeneo ambayo hayajapata. Kikao **kiliagiza** kuwa mapato yote yakusanywe kwa njia hiyo kama Serikali ilivyoagiza, aidha kwa Watendaji wa Kata wasioweza kutumia “POS” wapewe majukumu mengine ili kuweka watu wenye uwezo wa kutumia “POS” kwa lengo la kukusanya kikamilifu na kuongeza mapato ya Halmashauri.
- 4.13 **Utekelezaji** - Agizo lilizingatiwa, Ofisi ya Ugavi inaendelea na taratibu za manunuzi ya ‘POS’ . Aidha, mafunzo ya mara kwa mara yameendelea kutolewa kwa watumiaji wa ‘POS. Wajumbe walishauri kuwa mafunzo juu ya matumizi ya ‘POS’ yaendeleo kutolewa kwa watu mbalimbali ili watu wengi wawe na uelewa juu ya matumizi yake.
- 4.14 **Hoja Na. 5** Mjumbe alitoa hoja kuwa wafanyabiashara wanaosambaza mazao na kuni katika Shule za Sekondari watozwe ushuru kwa kuwa hakuna mahali wanapolipa ushuru huo. Kikao **kiliagiza** kuwa Idara ya Fedha na Biashara kwa kushirikisha Idara za Elimu, ifuatilie jambo hili kwa karibu ili mapato hayo yapatikane na taarifa itolewe kikao kijacho. Taarifa hii ihusishe pia wafanyabiashara wengine wanaotoa huduma nyingine za kishule tofauti na kuni na mazao.
- 4.15 **Utekelezaji** - Barua yenye Kumb. Na. KGR/KRG/ED/VOL.VI/255 ilitumwa kwa Wakuu wa Shule zote za Serikali zinazo hudumiwa na wazabuni ili wachangie mapato ya Halmashauri.
- 4.16 Pia kwenye kikao cha Idara cha kawaida cha tarehe 17/01/2017 Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara alitoa maelekezo kwa Wakuu wa Shule juu ya suala hili.
- 4.17 Hata hivyo, kwa mwezi Februari, 2017 jumla ya **TSh. 474,400.00** zimekusanywa ikiwa ni ushuru wa huduma zinazo tolewa na wazabuni katika shule.



- 4.18 Wajumbe walishauri kuwa shule binafsi pia zihusishwe ili ziweze kukusanya ushuru huo.
- 4.19 Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari pamoja na Afisa Biashara watembelee shule hizo za Sekondari, wafanye vikao na wahusika ili kuisitiza jambo hilo la kukusanya ushuru kutoka kwa wazabuni ikiwa ni pamoja na kukubaliana juu ya asilimia itakayo baki katika Shule za binafsi kwa ajili ya wakusanya ushuru hao.
- 4.20 Hoja Na. 6** Mjumbe alihoji ni kwanini mapato ya nyumba za Halmashauri hayaonekani. Ilifafanuliwa kuwa nyumba zote zilirudishwa Serikali Kuu na kwamba nyumba za Halmashauri zilizobaki ni 11 tu, ambapo wapangaji wanaendelea kuzilipia kupitia mfumo wa "LAWSON", isipokuwa watumishi wawili ambao mmojawapo mshahara wake haujahamishiwa Wilayani Karagwe na mwingine kiwango cha makato hakitoshi kuingiza makato mengine. Kikao **kiliagiza** kuwa suala la watumishi hao wawili litatuliwe haraka kwa kuwataka watumishi hao walipe fedha taslimu na taarifa itolewe kikao kijacho.
- 4.21 Utekelezaji** - Watumishi hao wawili wamefuatiliwa ambapo mmoja ameandikiwa barua yenye Kumb Na KGR/HWK/13329/38 ya tarehe 27/01/2017 ya kumtaka kulipa deni lake kiasi cha TSh. 831,360.00 na mtumishi wa pili amepewa notisi ya siku 30 yenye Kumb. Na. 10 GTZ /HWK/T.I.I/146 ya tarehe 17/02/2017 ya kumtaka kuhama katika nyumba hiyo na kulipa deni lake kiasi cha **TSh. 1,036,800.00.**
- 4.22 Wajumbe walishauri kuwa suala hilo liendeleo kufanyiwa kazi kwa kina.
- 4.23 Hoja Na. 4** Wakijadili taarifa hiyo, mjumbe alihoji juu ya uhalali wa gharama zilizotumika kukarabati vitanda na vifaa vingine kwa Idara ya Afya, takribani **TSh. 18,646,999.00** na **waliagiza** kuwa Mganga Mkuu alete mchanganuo wa matumizi ya fedha hiyo, na vifaa hivyo vikaguliwe wakati wa ukaguzi wa miradi.
- 4.24 Utekelezaji** - Orodha ya vifaa vilivyotengenezwa iliwasilishwa ikionesha matumizi ya vifaa hivyo kama vifaa vya jengo la upasuaji, vitanda, mashine na kitanda cha huduma ya meno. Orodha kamili na mchanganuo iliambatanishwa.
- 4.25 Wajumbe walishauri kuwa menejimenti iwe inajiridhisha na bei kabla ya kufanya manunuzi na kuhakikisha inapatikana bei rahisi.
- 4.26 Hoja Na. 9** Baada ya wajumbe kupitia mapendekezo ya mchoro wa soko jipya na kutoa ushauri, **waliazimia** kuwa ujenzi wa soko hilo utangazwe kwa Makampuni au watu binafsi wenye uwezo na kwamba mikataba yenye vigezo vya kisheria iandaliwe ili watu hao waruhusiwe kuanza ujenzi mapema mwezi wa tatu 2017.
- 4.27 Utekelezaji** -Taratibu zinaendelea.
- 4.28 Wajumbe walishauri kuwa ujenzi wa soko pamoja na kiwanja cha michezo, hayo yafanyike kwa kasi na kukamilika.

- 4.29 Aidha, wajumbe walishauri kuwa katika kuandaa makadirio ya gharama za ujenzi wa soko, mtu binafsi aliyekuwa amehusishwa awali katika kuandaa mchoro pia ashirikishwe katika kuandaa makadirio ya gharama za ujenzi.
- 4.30 **Hoja Na. 12** Ili kuendelea kuboresha ufaulu kwa shule zote za Msingi kikao **kiliazimia** kuwa iandaliwe taarifa inayoonesha idadi ya walimu (waliopo na walio masomoni), idadi ya wanafunzi na mikondo iliyopo kwa kila shule.
- 4.31 **Utekelezaji** - Azimio lilizingatiwa, na taarifa inayoonesha idadi ya walimu waliopo, walioko masomoni, idadi ya wanafunzi na mikondo iliandaliwa na kuambatanishwa.
- 4.32 **Hoja Na. 14** kuwa fedha za maafa zilizoletwa, zitolewe fedha zilizotumiwa awali kwa makubaliano kwamba Halmashauri itarejeshewa fedha hizo ili zifanye kazi zilizokusudiwa awali.
- 4.33 Wajumbe **waliazimia** kuwa kiasi cha fedha kinachodaiwa katika mfuko wa maafa kijulikane na kurejeshwa katika nafasi yake, watu mbali mbali waliofanya kazi za maafa walipwe fedha zao wanazo zidai ili mfuko wa maafa ufungwe na taarifa itolewe kikao kijacho.

## 5.0 **KUMB. NA. 100/2016/2017/8 - TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2017.**

- 5.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imekisia kukusanya na kutumia kiasi cha fedha jumla ya **TSh. 34,217,710,807.00**. Hata hivyo, kwa mwezi Januari, 2017 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imekusanya kiasi cha **TSh. 2,971,191,099.84** ambapo jumla ya mapato kwa mwezi Julai 2016 hadi Januari 2017 ni **TSh. 18,760,112,486.61** ambayo ni sawa na asilimia 54.83 ya lengo kwa mwaka.
- 5.2 Aidha, kwa mwezi Januari 2017, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imetumia jumla ya **TSh. 2,496,601,710.55** ambapo jumla ya matumizi kwa mwezi Julai, 2016 hadi Januari 2017 ni **TSh. 18,895,150,320.04** ambayo ni sawa na asilimia 51.31 ya lengo lake kwa mwaka.
- 5.3 Wakijadili taarifa hii, mjumbe alitoa ushauri kuwa fedha za vijiji na kata zinapopelekwa, Wah, Madiwani wapewe taarifa ili iwe rahisi katika kusimamia matumizi ya fedha hizo.
- 5.4 Kuhusu ukusanyaji wa ushuru wa madini, wajumbe walishauri kuwa magari yote yaainishwe ili yawe yanalipia kwa mwaka ili kuondoa usumbufu unaojitokeza katika usimamizi wa kila siku.
- 5.5 Kuhusu ukusanyaji wa kodi ya majengo, ushuru wa taka na ushuru wa madini, wajumbe **waliazimia** kuwa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo pamoja na Afisa Ardhi wakae kikao pamoja na Watendaji wa Kata zilizoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo ili kuweka mkakati wa pamoja juu ya ukusanyaji wa kodi ya majengo, Hoteli na ushuru wa madini.

- 5.6 Kuhusu upotevu wa mapato katika minada, wajumbe walisisitiza kuwa minada isimamiwe vizuri na kwamba siku ya minada ipewe kipaumbele ili kuhakikisha usimamizi wa kina unafanyika.
- 5.7 Wajumbe walijadili juu ya deni ambalo Halmashauri inadai kampuni ya CHICO na **kuazimia** kuwa iandaliwe orodha ya makampuni (wakandarasi) waliokwisha lipia ushuru wa huduma ili itumike kuhalalisha deni hilo la CHICO na kisha kampuni hiyo ifunguliwe kesi mahakamani na taarifa itolewe kikao kijacho.
- 5.8 Aidha, wajumbe walishauri kuwa Serikali ishauriwe kubadili sheria ya ushuru wa huduma ili makampuni yatakayo kuwa yanapewa kazi yaelekezwe kisheria kulipa ushuru wa huduma kwa Halmashauri moja kwa moja.
- 5.9 Kuhusu magari mbalimbali ya Halmashauri yaliyo chakaa, wajumbe **waliazimia** kuwa magari hayo yaombewe kibali ili yauzwe .
- 5.10 Aidha, wajumbe walishauri kuwa endapo taratibu za kuuza magari zitaonekana kuchelewa, Mhe. Mbunge ashirikishwe ili aweze kusaidia katika kufuatilia vibali hivyo.
- 5.11 Taarifa ilipitishwa.

**6.0 KUMB. NA. 101/2016/2017/8 - TAARIFA YA MANUNUZI NA BODI YA ZABUNI KWA KIPINDI CHA MWEZI JANUARI, 2017.**

- 6.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ilikisia kununua vifaa, kazi na huduma mbalimbali vyenye thamani ya **TSh. 5,181,938,618.70** kwa mwaka.
- 6.2 Kwa mwezi Januari 2017, Halmashauri ilikisia kununua vifaa, kazi na huduma vyenye thamani ya **TSh. 431,828,218.23** ambapo manunuzi halisi yaliyofanyika ni **TSh. 86,724,450.88** kwa Idara/Vitengo mbalimbali.
- 6.3 Taarifa ilipitishwa.

**7.0 KUMB. NA. 102/2016/2017/8 - TAARIFA YA HOJA ZA UKAGUZI WA NDANI ROBO YA PILI SEPTEMBER - DESEMBA, 2016/2017.**

- 7.1 Wakijadili taarifa ya hoja za ukaguzi, wajumbe walishauri kuwa majibu stahiki ya hoja hizo yawekwe.
- 7.2 Aidha, wajumbe walisisitiza kuwa taarifa yenye majibu kamili pamoja na viambatanisho vinavyotakiwa iwasilishwe katika kikao kijacho.
- 7.3 Taarifa ilipitishwa.

**8.0 KUMB. NA. 103/2016/2017/8 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA IDARA YA ELIMU SEKONDARI.**

- 8.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha Matokeo ya Kidato cha Nne 2016, ajali ya moto katika bweni la wavulana Kayanga Sekondari ambapo misaada mbali mbali ilikuwa imetolewa na Halmashauri, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya pamoja na Shule.

8.2 Taarifa ilipitishwa.

**9.0 KUMB. NA. 104/2016/2017/8- KUWASILISHA TAARIFA YA MAFUNZO YA UTUMIAJI NA UENDESHAJI WA TOVUTI MIKOA NA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA KWA WATAALAM WA TEHAMA NA HABARI YALIYOFANYIKA JIJINI MWANZA KUANZIA TAREHE 13/02/2017 HADI TAREHE 20/02/2017.**

9.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha malengo ya mafunzo hayo kuwa ni kuwawezesha Wataalam kutumia tovuti, kuimarisha mfumo wa mawasiliano Serikalini, upigaji picha kwa mfumo wa kidijitali, na kuhabarisha jamii kutumia vyombo mbali mbali vya habari.

9.2 Aidha, baada ya mafunzo hayo, Sekretarieti za Mikoa pamoja na Halmashauri zote zilipewa ofa na Wakala wa Serikali Mtandao ( EGA) ya mwaka mmoja ya kuhifadhi tovuti pasipo kulipia na kwamba baada ya mwaka mmoja wa ofa hiyo, Halmashauri itaendelea kulipia kiasi cha **TSh. 525,500.00** kwa mwaka.

9.3 Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walishauri kuwa Kitengo cha TEHAMA kihakikishe kinakusanya taarifa za matukio mbali mbali na kuziweka kwenye tovuti ya Halmashauri mara kwa mara ili kutoa taarifa kwa umma na kuelimisha jamii.

9.4 Taarifa ilipitishwa.

**10.0 KUMB. NA. 105/2016/2017/8 - TAARIFA YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA ROBO YA PILI, 2016/2017.**

10.1 Wakijadili taarifa za ukaguzi wa miradi, wajumbe **waliagiza** kuwa uandaliwe mfumo mmoja wa uwasilishaji taarifa za ukaguzi kwani mfumo unaotumika sasa unakuwa wa taarifa ndefu sana.

10.2 Pia wajumbe walishauri kuwa baada ya ukaguzi wa miradi timu zote zipate siku ya kufanya majumuisho.

10.3 Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa Mkuu wa Idara ya Ujenzi pamoja na Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi waende kukagua chumba cha darasa katika Shule ya Msingi Kakiro Kata ya Chanika kinachodaiwa kutokuwa na madirisha na kutoa ushauri.

**11.0 KUMB. NA. 106/2016/2017/8 - TAARIFA YA KIKAO KAZI KWA MAAFISA WA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU MIONGOZO YA MFUMO WA UPELEKAJI WA FEDHA ZA MAENDELEO KWENYE SERIKALI ZA MITAA ( LGCDG) TAREHE 1-3/02/2017 MWANZA.**

11.1 Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe **waliazimia** kuwa mwongozo wa fedha ya CDG upitiwe upya, vigezo vyote vifahamike ili fedha hizo zitumike kulingana na mwongozo.

- 11.2 Pia ilishauriwa kuwa mafunzo au semina ya Wah. Madiwani itakayofanyika, mwongozo, masharti na vigezo vya fedha hizo za CDG iwe ni miongoni mwa mambo yatakayofundishwa.
- 11.3 Kuhusu miradi viporo, wajumbe walishauri kuwa mkakati wa kumalizia miradi viporo uendelee na kwamba mfuko wa jimbo ujikite katika kumalizia miradi viporo na pia katika ugawaji wa fedha ziangaliwe nguvu za wananchi na michango yao iliyokwisha wekwa katika mradi husika.
- 11.4 Kuhusu usimamizi mbovu wa fedha zinazopelekwa ngazi za chini kwa ajili ya miradi mbali mbali wajumbe walishauri kuwa fedha hizo ziwe zinaambatana na barua ya maelekezo juu ya matumizi sahihi ya fedha hizo.
- 11.5 Aidha wajumbe walishauri kuwa kila mradi uwe na akaunti yake na kwamba barua iandikwe kwa Watendaji wa Kata na Vijiji kuwataka kuhakikisha kila mradi unakuwa na akaunti yake ili kurahisisha utekelezwaji wake.
- 11.6 Kuhusu utoroshwaji wa mifugo minadani, wajumbe **waliazimia** kuwa mabomba yaliyoko katika Kijiji cha Nyakayanja, yatumike kujengea uzio katika mnada wa Nyaishozi na kwamba yachukuliwe mabomba mengine kutoka Idara ya Maji, zitafutwe waya ili ujenzi wa uzio ufanyike katika mnada wa Nyaishozi na baadae Rukole.
- 11.7 Wajumbe walishauri kuwa utekelezaji huo uendeleo ili katika kikao kijacho wapewe taarifa. Aidha walishauri kuwa kiasi cha motisha ya mgambo wanaofanya kazi siku ya mnada kiboreshe ili kuendana na uhalisia wa kazi na matumizi yao siku hiyo.
- 11.8 Kuhusu makazi ya mtumishi anayekusanya ushuru katika kizuizi cha Kihanga, wajumbe walipendekeza kuwa Menejimenti isaidie kuboresha makazi ya mtumishi huyo.
- 11.9 Kuhusu mtumishi anayefanya kazi katika kizuizi cha Nyakasimbi, wajumbe walishauri kuwa Menejimenti iboreshe makazi yake kwa kumwekea umeme ili aweze kupata taa na mahali pa kuchajia' POS'.
- 11.10 Kuhusu malalamiko yaliyotolewa dhidi ya Mtendaji wa Kijiji cha Kafunjo wajumbe **waliazimia** kuwa Mtendaji huyo afuatiliwe ili kujua ukweli wa tuhuma zinazotolewa dhidi yake na kikao kijacho taarifa itolewe.
- 11.11 Wajumbe walitoa hoja kuwa katika Shule ya Msingi Kakiro katika Kata ya Chanika kuna chumba cha darasa kinachotumiwa na wanafunzi bila kuwa na madirisha.
- 11.12 Taarifa ilipitishwa.

**12.0 KUMB. NA. 107/2016/2017/8 - UTEKELEZAJI WA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI -TASAF AWAMU YA TATU KWA KIPINDI CHA MWEZI FEBRUARI - 2017.**

- 12.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na uhawilishaji wa fedha kwa walengwa, uhakiki wa wanafunzi na watoto ambao wako kliniki ili kuhakikisha kila mlengwa anapokea fedha stahiki kulingana na watoto alionao na

kuendelea kupokea rufaa za walengwa waliopendekezwa kuondolewa kwenye mpango.

12.2 Taarifa ilipitishwa.

**13.0 KUMB. NA. 108/2016/2017/8 - MAPENDEKEZO YA KUTOA MIKOPO KWA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA JANUARI - MACHI, 2017.**

13.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa vikundi vinavyoombewa kupewa mikopo ni vitatu (3). na kwamba fedha inayo kusudiwa kutolewa ni **TSh. 8,000,000.00**.

13.2 Aidha vikundi vilivyopendekezwa kupewa mikopo viliainishwa kama ifuatavyo;

1. JIPE MOYO - Kata ya Kiruruma **TSh. 1,500,000.00**.
2. KAYANGA YOUTH MODERN FUNITURES - Kata ya Kayanga **TSh. 5,000,000.00**.
3. YANGUA - Kata ya Rugu **TSh. 1,500.000.00**.

13.3 Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walishauri kuwa utoaji wa mikopo ujikite maeneo ya pembezoni kwani maeneo ya mjini hasa Kayanga yamekuwa yakipatiwa mikopo mara kwa mara na kwamba kipindi kijacho fedha hizo zielekezwe vijijini.

13.4 Taarifa ilipitishwa.

**14.0 OKUMB. NA. 109/2016/2017/8 - KUOMBA KIBALI CHA MATUMIZI YA TSH. 64,157,330.00 KUTOKA KATIKA VIFUNGU VYA MATUMIZI YA MRADI WA MDH CHINI YA SEKTA YA IDARA YA AFYA.**

14.1 Wajumbe walijadili taarifa hiyo na kuridhia kuwa fedha hizo zitumike kama zilivyoombwa.

14.2 Taarifa ilipitishwa.

**15.0 KUMB. NA. 110/2016/2017/8 - KUFUNGA KIKAO.**

15.1 Akifunga kikao, mwenyekiti aliwapongeza wajumbe wote kwa kuhudhuria na kujadili kwa pamoja taarifa mbalimbali zilizowasilishwa.

16.2 Kikao kilifungwa mnamo saa 12:00 jioni.

**TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO.**

Ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kutokana na kikao kilichoketi tarehe 24/03/2017 kuanzia saa 3:36 Asubuhi . Kikao kilichohudhuriwa nawajumbe 9 kati ya Kumi na wataalam waliohudhuria walikuwa ni 23.

Kikao kilizingatia agenda kama inavyooneshwa kwenye Dondoo zifuatazo.

**1.0 KUMB. NA. 112/2016/2017/9-KUTHIBITISHA DONDOO.**

1.1 Wajumbe walijadili dondoo zilizowasilishwa na kuongeza zifuatazo:

1. Maombi ya idhini ya kutumia fedha za Miradi ya Maji zilizokuwa nje ya Bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017.
2. Taarifa juu ya hali ya mahindi yaliyopandwa mwishoni mwa mwezi Januari na mwanzoni mwa mwezi Februari 2017.
3. Baada ya kuongeza dondoo hizo, wajumbe walikubaliana kuwa dondoo hizo ndizo zijadiliwe.

**2.0 KUMB. NA. 113/2016/2017/9 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 28/02/2017.**

- 2.1 Muhtasari ulisomwa na kisha wajumbe walikubaliana kuwa muhtasari huo uwe kumbukumbu sahihi za vikao hivi na kisha ulisainiwa na Mwenyekiti.

**3.0 KUMB. NA 114/2016/2017/9 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 28/02/2017.**

- 3.1 **Hoja na 1-** Wajumbe **waliagiza** kuwa ufuatiliaji juu ya suala hilo uendeleo kufanyika, Watendaji wa Kata na Vijiji wabaini minara yote iliyopo katika maeneo yao na washirikishe viongozi wenzao katika vikao vya WDC na Serikali za Vijiji kisha iandaliwe taarifa ya maandishi kwa kila eneo ambayo itaonesha ni lini minara hiyo imeanza kufanya kazi, ni ya kampuni gani na iko kwenye ardhi ya nani.
- 3.2 Baada ya kupatikana kwa taarifa hiyo, wajumbe walishauri kuwa TAMISEMI waandikiwe barua kufahamishwa juu ya madai ya ushuru wa huduma ambao Halmashauri inadai kutoka kwa Makampuni ya Simu na kwamba barua hiyo apewe nakala Katibu Mkuu Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi.
- 3.3 **Utekelezaji** - Azimio limetekelezwa na taarifa imeambatanishwa, aidha barua yenye KUMB. Na. KGR/HWK/T.33/VOL.1 /91 ya tarehe 17/03/2017 kwa mameneja wote wa minara iliyotajwa katika taarifa kuwataka walipe ushuru wa huduma.
- 3.4 Hivyo wasipotii agizo hilo, barua itaandikwa kwenda TAMISEMI na Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi kwa ajili ya ufuatiliaji zaidi.
- 3.5 **Hoja na 2** - Aidha wajumbe **waliazimia** kuwa Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari pamoja na Afisa Biashara watembelee Shule hizo za Sekondari, wafanye vikao na wahusika ili kusesitiza jambo hilo la kukusanya ushuru kutoka kwa wazabuni ikiwa ni pamoja na kukubaliana juu ya asilimia itakayobaki katika Shule za binafsi kwa ajili ya wakusanya ushuru hao.
- 3.6 **Utekelezaji** - Barua yenye Kumb Na KGR/HWK/T.22/1/VOL.VII/68 ya tarehe 28/02/2017 ilitumwa kwa Wakuu wa Shule zisizo za Serikali ikiwataka kuwasilisha orodha ya wazabuni.
- 3.7 Pia, Mkuu wa Idara ya Elimu Sekondari, Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara pamoja na Afisa Biashara, wametembelea Shule za Sekondari na kuongea na

- Wakuu wa Shule hizo na kuwapa utaratibu wa kukusanya ushuru wa huduma kutoka kwa wazabuni.
- 3.8 Wakiijadili hoja hiyo wajumbe **waliagiza** kuwa taarifa hii iwasilishwe tena (kwa maandishi) ikionesha ushuru huo unatakiwa kulipwa na mkandarasi yeyote anayefikisha mzigo shuleni kama ushuru wa mazao sio ushuru wa huduma. Aidha viwekwe viwango kamili vya tozo hiyo na pia kioneshwe kiwango cha motisha kwa Shule kama wakala.
- 3.9 **Hoja na 3 - Hoja Na. 14** kuwa fedha za maafa zilizoletwa, zitolewe fedha zilizotumiwa awali kwa makubaliano kwamba Halmashauri itarejeshewa fedha hizo ili zifanye kazi zilizokusudiwa awali.
- 3.10 Wajumbe **waliazimia** kuwa kiasi cha fedha kinachodaiwa katika Mfuko wa Maafa kijulikane na kurejeshwa katika nafasi yake, watu mbali mbali waliofanya kazi za maafa walipwe fedha zao wanazozidai ili mfuko wa maafa ufungwe na taarifa itolewe kikao kijacho.
- 3.11 **Utekelezaji** - Fedha zilizotumika kwenye shughuli za maafa ni TSh. 23,518,470/= . Kati ya hizo TSh. 12,499,520/= ni mafuta lita 5,830 na TSh. 11,018,950/= ni posho, chakula, gharama ya kununua mifuko ya kugawa chakula pamoja na mchango wa Halmashauri. Tarehe 14/3/2017 limeandikwa dokezo kwa Mkurugezini Mtendaji kuomba kurejesha fedha hizo.
- 3.12 Wakiijadili taarifa hiyo, wajumbe walishauri kuwa iandikwe barua Ofisi ya Mkuu wa Mkoa ikionesha mchanganuo wa madai hayo na kuomba kurejeshewa fedha hizo ili kuondoa hoja ya ukaguzi.
- 3.13 **Hoja na 4** - Kuhusu madai ya ushuru wa huduma unaopaswa kulipwa na kampuni ya CHICO, wajumbe **waliazimia** kuwa viandaliwe vielelezo vya wakandarasi waliolipa ushuru wa huduma ili kuhararisha madai hayo kisha kesi ifunguliwe dhidi ya Kampuni ya CHICO na kikao kijacho taarifa itolewe.
- 3.14 **Utekelezaji** - Mchakato wa kisheria unaendelea.
- 3.15 **Hoja na 5** - Kuhusu ukusanyaji wa kodi ya majengo, ushuru wa taka na ushuru wa madini, wajumbe **waliazimia** kuwa Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo pamoja na Afisa Ardhi wakae kikao pamoja na Watendaji wa Kata zilizoko katika Mamlaka ya Mji Mdogo ili kuweka mkakati wa pamoja juu ya ukusanyaji wa kodi ya majengo, Hoteli na ushuru wa madini.
- 3.16 **Utekelezaji** - Kikao hicho kilifanyika tarehe 02/03/2017 na mikakati iliyowekwa ni pamoja na kutangaza redioni kuhusu ulipwaji wa ushuru husika na kutumia gari ya matangazo. Pia Viongozi wa Kata wasimamie na asilimia 10 irudi Ofisi za Kata kwa ajili ya kusaidia shughuli za Ofisi.
- 3.17 **Hoja na 6** - Kuhusu magari mbali mbali ya Halmashauri yaliyochakaa, wajumbe **waliazimia** kuwa magari hayo yaombewe kibali ili yauzwe.
- 3.18 **Utekelezaji** - Barua yenye kumb. Na. KGR/HWK/T.2/19/VOL/61 ya tarehe 29/06/2016 iliandikwa kwa Katibu Mkuu, Wizara ya Fedha na Mipango kuomba



- kibali kwa magari mawili ambayo yalikuwa yameainishwa awali ambayo ni STJ 3331 na SM 2455 na kujibiwa kwa barua yenye Kumb Na. EB/AG/APT.GEN/16/VOL.V/85 ya tarehe 24/11/2016.
- 3.19** Barua nyingine yenye Kumb. Na. KGR/HWK/T.2/19/VOL.VII/74 ya tarehe 31/10/2016 iliongeza magari mengine ambayo ni DFP 2401, SM 3122, STJ 3331 na DFP 4227 na kisha kukumbushia kwa barua ya Kumb. Na. KGR/HWK/T.35/15/VOL.1/04 ya tarehe 01/02/2017.
- 3.20 Hoja Na. 7-** Wakijadili taarifa za ukaguzi wa miradi, wajumbe **waliagiza** kuwa uandaliwe mfumo mmoja wa uwasilishaji taarifa za ukaguzi kwani mfumo unaotumika unakuwa wa taarifa ndefu sana.
- 3.21 Utekelezaji** - Azimio limezingatiwa, taarifa za ukaguzi wa miradi ujao, mfumo bora wa uwasilishaji taarifa utatumiwa kama ilivyoagizwa na Kamati.
- 3.22 Hoja Na. 8** - Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe **waliazimia** kuwa mwongozo wa fedha ya CDG upitiwe upya, vigezo vyote vifahamike ili fedha hizo zitumike kulingana na mwongozo.
- 3.23 Utekelezaji** - Mwongozo wa fedha za LGCDG wa mwaka 2014 unaelekeza kuwa katika asilimia 100 ya fedha zote, asilimia 10 ni kwa ajili ya kujenga uwezo, asilimia 80 ni kwa ajili ya miradi na asilimia 10 ni kwa ajili ya ufuatiliaji.
- 3.24 Aidha, mgao huo hutegemea idadi ya watu ( IPF) Indicative, Planning Figure
- 3.25 Wajumbe **waliazimia** kuwa mwongozo kamili wa matumizi ya fedha hizo uwasilishwe ikiwa ni pamoja na taarifa ya matumizi ya fedha hizo na fedha za kujenga uwezo (Capacity buiding) na kwamba taarifa kamili itolewe kikao kijacho.
- 3.26 Hoja Na. 9** - Kuhusu malalamiko yaliyotolewa dhidi ya Mtendaji wa Kijiji cha Kafunjo wajumbe **waliazimia** kuwa Mtendaji huyo afuatiliwe ili kujua ukweli wa tuhuma zinazotolewa dhidi yake na kikao kijacho taarifa itolewe.
- 3.27 Utekelezaji** - Taarifa iliwasilishwa.
- 3.28 Hoja Na. 10** - Aidha, wajumbe **waliazimia** kuwa Mkuu wa Idara ya Ujenzi pamoja na Mkuu wa Idara ya Elimu Msingi waende kukagua chumba cha darasa katika Shule ya Msingi Kakiro Kata ya Chanika kinachodaiwa kutokuwa na madirisha na kutoa ushauri.
- 3.29 Utekelezaji** - Eneo limekaguliwa mnamo tarehe 16/3/2017. Gharama za madirisha 20 ya chuma na lenta juu ya madirisha hayo katika vyumba 6 vya madarasa ni TSh. 4,970,000/= . Zinahitajika TSh. 15,361,500/= . Mchanganuo wa gharama hizo uliambatanishwa.
- 3.30 Wajumbe **waliazimia** kuwa kwa kuwa Shule hiyo ya Kakiro ni mali ya wananchi na Kijiji, waelekezwe kufanya ukarabati wa darasa hilo na kwamba wakitaka msaada wa kiutaalam wawasiliane na Idara ya Ujenzi.
- 3.31 Hoja Na. 11-** Kuhusu utoroshwaji wa mifugo minadani, wajumbe **waliazimia** kuwa mabomba yaliyoko katika Kijiji cha Nyakayanja, yatumike kujengea uzio katika mnada wa Nyaishozi na kwamba yachukuliwe mabomba mengine kutoka

Idara ya Maji, zitafutwe waya ili ujenzi wa uzio ufanyike katika mnada wa Nyaishozi na badae Rukole.

**3.32 Utekelezaji** - Azimio lilizingatiwa, taarifa iliambatanishwa.

**4.0 KUMB. NA. 115/2016/2017/9 - TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI FEBRUARI, 2017.**

4.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/2017, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imekisia kukusanya na kutumia kiasi cha fedha **TSh. 34,339,722,796.91**

4.2 Hata hivyo, kwa mwezi Februari, 2017 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imekusanya kiasi cha **TSh. 1,956,376,519.51** ambapo jumla ya mapato kwa mwezi Julai hadi Februari 2017 ni **TSh. 20,423,489,006.12** ambayo ni sawa na asilimia 59.65 ya lengo zima kwa mwaka.

4.3 Kwa upande wa matumizi, kwa mwezi Februari 2017, Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imetumia Jumla ya **TSh. 2,422,276,747.25** ambapo Jumla ya matumizi kwa mwezi Julai hadi Februari, 2017 ni **TSh. 21,016,924,822.56** ambayo ni sawa na asilimia 56.99.

4.4 Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walieleza kuwa baadhi ya Wakuu wa Idara hawawashirikishi Wasaidizi wao na kuongeza kuwa Kamati itakuwa inakagua kuona kama Idara zinafanya vikao vya kiutendaji ikiwa ni pamoja na kukagua mihtasari ya vikao hivyo.

4.5 Kuhusu upande wa matumizi, wajumbe walisisitiza kuwa taarifa ya fedha za Miradi ya Maendeleo zilizopelekwa inabidi iwe sehemu ya taarifa ya matumizi.

4.6 Mjumbe alitoa hoja kuwa kuna watu wanaovamia misitu na kufanya shughuli za kilimo katika sehemu mbali mbali ambapo ilifafanuliwa kuwa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya tayari inashughulikia suala hilo na Operation inaendelea kufanyika.

**5.0 KUMB. NA 116/2016/2017/9 - TAARIFA YA MANUNUZI NA BODI YA ZABUNI KWA MWEZI FEBRUARI, 2017.**

5.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/2017 Halmashauri ilikisia kununua vifaa, kazi na huduma mbali mbali vyenye thamani ya **TSh. 5,181,938,618.70** kwa mwaka .

5.2 Kwa mwezi Februari, 2017 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe ilikisia kununua vifaa, kazi na huduma mbali mbali vyenye thamani ya **TSh. 431,828,218.23** hata hivyo, manunuzi halisi yaliyofanyika ni TSh. 29,917,876.00 kwa Idara na Vitengo.

5.3 Taarifa ilipitishwa.

**6.0 KUMB. NA 117/2016/2017/9 - KUWASILISHA MAJIBU YA HOJA ZA UKAGUZI WA NDANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA PILI 2016/2017.**

- 6.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha jumla ya hoja 15 ambapo hoja 6 ni za kipindi cha nyuma na hoja 9 ni za kipindi cha robo ya pili.
- 6.2 **Hoja Na. 8.1** juu ya kutokusanya ushuru wa huduma kwa baadhi ya wafanya biashara wa vituo vya mafuta **TSh. 6,550,000.**
- 6.3 Wajumbe walishauri kuwa uhakiki juu ya hoja hiyo ufanyike na hatua zichukuliwe.
- 6.4 **Hoja Na 8.7** juu ya kuchelewa kuendeleza eneo la Kishao - Bugene baada ya kumilikiwa kisheria.
- 6.5 Ilifafanuliwa kwamba tayari CMT imeafiki kwamba fedha zilizoletwa kwa ajili ya kuendeleza uwanja wa mpira, kitengwe kiasi cha fedha kitakacho tumika kusawazisha eneo hilo la stendi ya Kishao.
- 6.6 **Hoja Na 8.1** Juu ya kukosekana kwa hati 54 za malipo za **TSh. 493,041,972.72**
- 6.7 Ilifafanuliwa kuwa mtu anayehusika na masuala ya cheki ni mmoja na kwamba ataongezewa mtu mwingine ili kuhakikisha kumbukumbu zinatunzwa vizuri.
- 6.8 Wajumbe walisisitiza kuwa majibu ya hoja yawekwe na kikao kijacho hoja zote ziwe zimejibiwa.
- 6.9 **Hoja Na. 8.9** juu ya matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo yasiyozingatia mwongozo.
- 6.10 Wajumbe walisisitiza kuwa matumizi ya fedha za Mfuko wa Jimbo yazingatie mwongozo na si vinginevyo.
- 6.11 Taarifa ilipitishwa.

**7.0 KUMB. NA. 118/2016/2017/9 - MAOMBI YA IDHINI YA KUTUMIA FEDHA ZA MIRADI YA MAJI ZILIZOKUWA NJE YA BAJETI YA MWAKA WA FEDHA 2016/2017.**

- 7.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 iliyoidhinishwa na Bunge, Miradi ya Maji ilipangiwa kupokea na kutumia kiasi cha **TSh. 338,070,000.00** ikiwa ni fedha za kuendeleza ujenzi wa miundombinu ya maji.
- 7.2 Kwa kipindi cha Julai 2016, hadi Machi 2017 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imepokea jumla ya **TSh. 673,803,738.11** kwa ajili ya matumizi mbali mbali.
- 7.3 Kwa kuwa Halmashauri imepokea fedha zaidi ya makisio yaliyoidhinishwa, Idara iliomba idhini ya kutumia fedha zilizoongezeka kwa kazi zilizoelekezwa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa miundombinu ya maji mradi wa Nyakakika **TSh. 528,559,507.70**, fedha za usimamizi na usajili wa vikundi vya watumia maji **TSh. 18,236,115.71**, fedha za kampeini ya usafi wa mazingira **TSh. 13,000,000.00** na fedha za ujenzi wa miundombinu ya maji mradi wa Kigorogoro **TSh. 114,008.114.70** ambapo jumla ni **TSh. 673,803,738.11.**
- 7.4 Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango waliridhia matumizi ya fedha hizo.
- 7.5 Taarifa ilipitishwa.

**8.0 KUMB. NA 119/2016/2017/9 - TAARIFA JUU YA HALI YA MAHINDI YALIYOPANDWA MWISHONI MWA MWEZI JANUARI NA MWANZONI MWA MWEZI FEBRUARI.**

- 8.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa katikati ya mwezi Februari, 2017 yalianza kutoka malalamiko wakulima wakidai kuwa mbegu za seedCo Tumbili zilikuwa mbaya na kwamba zinaota kwa kunyong'onyea na zinashambuliwa sana na wadudu.
- 8.2 Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walisisitiza kuwa kiwepo kipindi cha redio ili kuendelea kutoa elimu kwa wakulima juu ya kutibu ugonjwa huo na msimu bora wa kulima mahindi.
- 8.3 Taarifa ilipitishwa.

**9.0 KUMB. NA 120/2016/2017/9 - KUFUNGA KIKAO.**

- 9.1 Akifunga kikao, Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe wote kwa kuchangia taarifa zilizowasilishwa na alisisitiza kuwa Wakuu wa Idara wafanye kazi kwa kuwashirikisha watu walioko chini yao ili kuweka uelewa wa pamoja ikiwa ni pamoja na kufanya vikao vya Idara.
- 9.2 Kikao kilifungwa mnamo saa 7:30 Mchana.

**TAARIFA YA KAMATI YA FEDHA, UONGOZI NA MIPANGO.**

Ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Fedha, Uongozi na Mipango kutokana na kikao kilichoketi tarehe 20/04/2017 kuanzia saa 4:56 asubuhi . Kikao kilichohudhuriwa na wajumbe 9 kati ya kumi na wataalam waliohudhuria walikuwa ni 24.

Kikao kilizingatia agenda kama inavyooneshwa kwenye Dondoo zifuatazo:

**1.0 KUMB. NA.124/2016/17/10 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 24/03/2017.**

- 1.1 **Hoja na 1** - Wakijadili hoja hiyo juu ya kukusanya ushuru wa huduma katika Shule za Sekondari, wajumbe **waliagiza** kuwa taarifa hii iwasilishwe tena (kwa maandishi) ikionesha ushuru huo unatakiwa kulipwa na mkandarasi yeyote anayefikisha mzigo shuleni kama ushuru wa mazao sio ushuru wa huduma. Aidha viwekwe viwango kamili vya tozo hiyo na pia kioneshwe kiwango cha motisha kwa Shule, kama wakala.
- 1.2 **Utekelezaji** - Wazabuni wanaopeleka chakula shuleni wanakuwa wameshalipia ushuru wa mazao. Kinacholipwa shuleni ni ushuru wa huduma ambapo huwa unalipwa.
- 1.3 Kuhusu kubakiza motisha shuleni sheria hairuhusu kubakiza kiasi chochote.
- 1.4 Wakijadili hoja hii, wajumbe walieleza kuwa Menejimenti haikutekeleza kama kikao kilivyoagiza. Hivyo **azimio** hilo litekelezwe upya kwa Shule za Sekondari na Msingi, na taarifa iwasilishwe kikao kijacho.

- 1.5 **Hoja na 2** - Wajumbe **waliazimia** kuwa kwa kuwa Shule hiyo ya Kakiro ni mali ya wananchi na kijiji, waelekezwe kufanya ukarabati wa madarasa hayo na kwamba wakitaka msaada wa kitaalam wawasiliane na Idara ya Ujenzi.
- 1.6 **Utekelezaji** - Azimio limetekelezwa. Uongozi wa Shule umeandikiwa barua yenye Kumb. Na. KA.04/02/030/34 ya tarehe 12/04/2017 kwa ajili ya utekelezaji.
- 1.7 Wakiijadili hoja hiyo, wajumbe walitaka kujua kama utekelezaji umeanza na ilifafanuliwa kuwa tayari wameitisha kikao kwa ajili ya kuanza utekelezaji wa suala hilo.
- 1.8 **Hoja na 3** - Wajumbe **waliazimia** kuwa mwongozo kamili wa matumizi ya fedha hizo za LGDG uwasilishwe ikiwa ni pamoja na taarifa ya matumizi ya fedha hizo na fedha za kujenga uwezo (Capacity buiding) na kwamba taarifa kamili itolewe kikao kijacho.
- 1.9 **Utekelezaji** - Mwongozo wa matumizi ya fedha za LGDG utatolewa kwenye kikao ikiwa ni pamoja na maandalizi ya mafunzo.
- 1.10 Wajumbe walitaka kujua hatua iliyofikiwa katika mradi wa ujenzi wa uwanja wa mpira wa miguu. Ilifafanuliwa kuwa tayari hatua za kutafuta mkandarasi zinaendelea.

## **2.0 KUMB. NA.125/2016/17/10 - TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA ROBO YA TATU, JANUARI - MACHI, 2017.**

- 2.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri ilikisia kukusanya na kutumia kiasi cha fedha chenye jumla ya TSh. 34,771,925,911.65 hata hivyo kwa mwezi Machi, 2017 Halmashauri ya Wilaya imekusanya kiasi cha TSh. 2,659,526,013.23 ambapo jumla ya mapato Julai 2016 hadi mwezi Machi 2017 ni jumla ya TSh. 23,376,065,020.34 ambayo ni sawa na 67.23%.
- 2.2 Kwa upande wa matumizi kwa mwezi Machi 2017 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imetumia jumla ya TSh. 2,837,318,827.13 ambapo jumla ya matumizi kwa mwezi Julai 2016 hadi mwezi Machi 2017 ni TSh. 24,216,773,540.69 ambayo ni sawa na 64.77% ya lengo kwa mwaka.
- 2.3 Wakiijadili taarifa hiyo wajumbe walishauri kuwa sheria ndogo ya madini ya Mamlaka ya Mji Mdogo ifanyiwe kazi na kukamilika mapema ili isaidie katika kukusanya mapato.
- 2.4 Wajumbe walishauri kuwa makadirio ya makusanyo ya mapato yawe yanapangwa kulingana na uhalisia wa vyanzo vya mapato kwani inaonekana makadirio ni makubwa kuliko mapato yenyewe. Aidha walisisitiza kuwa kila Idara ihakikishe inachangia katika kusimamia suala la ukusanyaji wa mapato.
- 2.5 Mjumbe alitoa hoja kwamba Mamlaka ya Mji Mdogo inashindwa kukusanya vizuri kutokana na kukosa mashine ya kielektroniki ya kukusanyia mapato. Iisisitiza kuwa Menejimenti itoe mashine hizo ili Mamlaka ya Mji Mdogo iweze kukusanya mapato kwa urahisi.

- 2.6 Wajumbe **waliazimia** kuwa sheria ndogo za Halmashauri zifuatiliwe ngazi ya Mkoa ili kufanya marekebisho yanayotakiwa na kuhakikisha zinakamilika haraka kabla ya mwaka wa fedha 2016/17 kumalizika.
- 2.7 Wajumbe walihoji juu ya kusuasua katika kutenga fedha za Wanawake na Vijana. Ilifafanuliwa kuwa kwa sasa shughuli zote za Halmashauri zinategemea mapato ya ndani yaani (own source), kwani hakuna ruzuku (OC) zinazoletwa. Wajumbe walishauri kuwa pindi fedha hizo zitakapoletwa zirejeshwe akaunti ya mapato ya ndani na kupelekwa kwenye mfuko wa wanawake na vijana.
- 2.8 Wajumbe **waliazimia** kuwa asilimia kumi ya wanawake na vijana itengwe kuanzia mwezi wa nne mwaka 2017 na pia mkakati wa kupunguza deni la nyuma uandaliwe na deni hilo lianze kupunguzwa.
- 2.9 Wajumbe walisisitiza kuwa Idara zinazoingiza kwa wingi mapato ya ndani kama Kilimo na Mifugo ziwezeshe ikiwa ni pamoja na kumwezesha Mwanasheria ili aweze kusimamia kesi mbali mbali.
- 2.10 Taarifa ilipitishwa.

**3.0 KUMB. NA. 126/2016/17/10 - TAARIFA YA MANUNUZI NA BODI YA ZABUNI KWA KIPINDI CHA JANUARI - MACHI, 2017.**

- 3.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri ilikisia kununua vifaa, kazi na huduma mbali mbali vyenye thamani ya TSh. 5,181,938,618.70 kwa mwaka. Ambapo kwa mwezi machi 2017 Halmashauri ilikisia kufanya manunuzi ya TSh. 431,828,212.23 ambapo manunuzi halisi yaliyofanyika ni yenye thamani ya TSh. 154,224,822.59 ambayo ni sawa na asilimia 35.7.
- 3.2 Kwa robo ya tatu Halmashauri ilikisia kununua vifaa/huduma mbali mbali vyenye thamani ya TSh. 1,295,484,654.69 ambapo manunuzi ya kawaida yaliyofanyika ni yenye thamani ya TSh. 320,173,149.47 ambayo ni sawa na asilimia 24.7.
- 3.3 Taarifa ilipitishwa.

**4.0 KUMB NA.127/2016/17/10 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MPANGO WA KUNUSURU KAYA MASKINI KWA ROBO YA TATU, JANUARI - MACHI, 2017.**

- 4.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa uhawilishaji wa fedha katika awamu hii umefanyika kwa dirisha la Januari - Februari na Machi - April 2017 katika Vijiji 54 ambapo wanufaika 9,292 na 9,100 waliletewa fedha zao. Katika dirisha la Januari - Februari jumla ya walengwa 139 hawakulipwa ruzuku zao na jumla ya TSh. 8,056,000.00 zilirejeshwa TASAF Makao Makuu kama ulivyo utaratibu.
- 4.2 Wakijadili taarifa hiyo wajumbe walitaka kujua sababu za baadhi ya walengwa kutopokea fedha zao. Ilifafanuliwa kuwa ni kwa sababu ya kutofika siku ya mgao.

4.3 Wajumbe **waliazimia** kuwa Mratibu TASAF awasiliane na TASAF Makao makuu ili watoe taarifa mapema na wananchi wapate taarifa mapema waweze kuhudhuria na kupatiwa fedha zao siku ya mgao.

4.4 Taarifa ilipitishwa.

**5.0 KUMB NA.128/2016/17/10 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA KITENGO CHA UCHAGUZI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU, JANUARI - MACHI, 2017.**

5.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kufuatilia kesi za uchaguzi mbali mbali zilizopo mahakamani, kuhudhuria vikao mbali mbali na kuratibu nafasi wazi za viongozi wa Kata, Vijiji na Vitongoji.

5.2 Wakijadili taarifa hii, wajumbe walitoa hoja kuwa kuna baadhi ya watu wanaoteuana kinyume cha sheria kushika nyadhifa mbali mbali pindi viongozi husika wanapofariki au kufukuzwa uanachama.

5.3 Wajumbe **waliazimia** kuwa mwongozo utolewe kwa ngazi zote za msingi kuonesha mfumo unaotumika pale kiongozi anapofariki au kufukuzwa uanachama.

5.4 Taarifa ilipitishwa.

**6.0 KUMB. NA. 128/2016/17/10 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA MAMLAKA YA MJI MDOGO KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU JANUARI - MACHI, 2017.**

6.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na ukusanyaji wa ushuru kwa mujibu wa sheria ndogo za Mamlaka, usimamiaji wa usafi wa Mji na uzoaji wa taka ngumu, kusikiliza matatizo ya wananchi, kuitisha vikao vya kisheria na kiutendaji.

6.2 Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walihoji juu ya ukusanyaji hafifu wa mapato ya Mamlaka ya Mji Mdogo. Ilifafanuliwa kuwa mapato yanakuwa hafifu kutokana na kutokuwa na 'POS' za kutosha kwa maeneo ya kukusanyia mapato. Kikao kilisitiza kuwa Menejimenti ihakikishe upatikanaji wa 'POS' kwa Mamlaka ya Mji Mdogo ili kuwezesha ukusanyaji wa mapato.

**7.0 KUMB. NA. 129/2016/17/10 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI JULAI - MACHI, 2017.**

7.1 Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri imeidhinishwa kiasi cha TSh. 5,643,393,738.61 ili kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo.

7.2 Kwa kipindi cha Julai - Machi 2016/17 Halmashauri ilipokea fedha kiasi cha TSh. 6,060,488,172.67 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Ambapo katika fedha hizo kiasi cha TSh. 1,413,011,969.54 ni bakaa ya mwaka 2015/16 na TSh.

4,647,476,204.13 zimepokelewa katika kipindi cha Julai - Machi 2017 sawa na asilimia 82.4 ya makisio kwa mwaka wa fedha 2016/17.

- 7.3 Wakiijadili taarifa hiyo, wajumbe **waliazimia** katika ukaguzi wa miradi utakaofanyika mwezi wa tano 2017, mradi wa ujenzi wa vyoo katika Shule ya Sekondari Nono uwekwe kwenye ratiba ya ukaguzi.
- 7.4 Kuhusu matumizi ya fedha za kifungu cha Ulinzi na Usalama katika bajeti kikao **kiliazimia** kuwa Menejimenti ilete mchanganuo wa matumizi ya kifungu hicho, ikiwa ni pamoja na kufafanua sababu za kifungu hicho zaidi ya makadirio.
- 7.5 Taarifa iliipitishwa.

#### **8.0 KUMB. NA. 130/2016/17/10 - TAARIFA YA IDARA YA UTUMISHI NA UTAWALA KWA ROBO YA TATU JANUARI - MACHI, 2017.**

- 8.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha vikao vya kisheria vilivyofanyika kwa robo ya tatu ngazi ya Kata na Vijiji na watumishi walioondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara na taarifa ya upimaji wa wazi wa utendaji kazi (OPRAS).
- 8.2 Wakiijadili taarifa hiyo wajumbe walisisitiza kuwa Kata au Vijiji watakaoshindwa kuitisha na kufanya vikao vya kisheria waondolewe kwenye mpango wa ruzuku.
- 8.3 Kuhusu taarifa ya upimaji wa wazi wa utendaji kazi (OPRAS), wajumbe **waliazimia** kuwa Idara itakayokuwa haijawasilisha taarifa hiyo kwa Idara ya Utumishi na Utawala hadi kufikia kikao kijacho, iwasilishwe kwenye kikao.
- 8.4 Taarifa ilipitishwa.

#### **9.0 KUMB. NA. 131/2016/17/10 - TAARIFA YA UKAGUZI WA NDANI ROBO YA TATU JANUARI - MACHI, 2016/17.**

- 9.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha jumla ya hoja 14, ambapo hoja nne zilikuwa ni za kipindi cha nyuma na 10 za robo ya tatu.
- 9.2 Wakiijadili taarifa hii, wajumbe walisisitiza kuwa Menejimenti ijibu hoja hizo kwa ukamilifu na majibu ya hoja hizo yawasilishwe kwenye kikao kijacho.
- 9.3 Kuhusu akaunti za miradi kuchanganyika na fedha za ruzuku katika Shule, wajumbe walisisitiza kuwa jambo lifanyiwe kazi kwa kutenganisha akaunti hizo ili kuondoa utata katika matumizi ya fedha.
- 9.4 Taarifa ilipitishwa.

#### **10.0 KUMB. NA. 131/2016/17/10 - KUFUNGA KIKAO.**

- 10.1 Akifunga kikao Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa kujadili taarifa zote kwa umakini.
- 10.2 Kikao kilifungwa mnamo saa 9:15 alasiri.



Wakizijadili taarifa hizo mjumbe alihoji juu ya baadhi ya vikundi kupata mkopo zaidi ya mara moja na wengine kukosa. Ilifafanuliwa kwamba suala hilo lilijitokeza mara moja kwa Kata ya Kituntu na kikundi hicho kina watu zaidi ya 400.

Wajumbe walisisitiza kuwa taarifa ziwe zinatolewa pindi vitabu vinapopelekwa kwenye Kata kwa ajili ya kukusanya michango mbali mbali.

kuhusu baadhi ya watumishi kupata changamoto pale POS zinapotoa risiti zisizo sahihi na kusababisha mkanganyiko katika mapato halisi yaliyokusanywa. Ilifafanuliwa kuwa mtumishi atakayekutwa na changamoto hiyo aripoti Idara ya Fedha akiwa na risiti hizo.

Mjumbe alitoa hoja kwamba POS zilizopo kwa sasa hazitoshi kukusanya mapato ya Halmashauri katika maeneo yote. Ilifafanuliwa kuwa POS zitaendelea kununuliwa katika bajeti ya mwaka ujao wa fedha.

Mjumbe alitaka kujua kama orodha ya minara imeandaliwa na majina ya wamiliki. Ilifafanuliwa kuwa orodha hiyo imeandaliwa na ipo kwa Mkuu wa Idara ya Utumishi na Utawala, ikihusisha minara iliyopo kwenye Ardhi ya Serikali.

Kuhusu ushuru wa huduma ya minara unaopaswa kulipwa na kampuni ya **htt** wajumbe walishauri kuwa Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara afuatilie ushuru huo kwa kampuni hiyo.

Kuhusu ahadi ya Kampuni ya Halotel kuweka huduma ya mtandao kwenye Ofisi za Umma wajumbe waliazimia kuwa ufuatiliaji wa jambo hilo ufanyike na taarifa itolewe.

Kuhusu suala la ukusanyaji wa mapato ngazi ya Kata wajumbe walishauri kuwa Kamati za Mapato za Kata zifanye kazi chini ya WDC na muundo wa Kamati hizo utolewe kwa Waheshimiwa Madiwani.

Kuhusu suala la ujenzi wa soko na uwanja wa mpira wajumbe walishauri kuwa utumike mfumo wa PPP ili kurahisha utekelezaji wa jambo hilo kwa muda mfupi.

Kuhusu ukaguzi wa vitabu vya kukusanyia michango mbali mbali kwa ngazi za Vijiji na Kata, wajumbe walishauri kuwa mrejesho uwe unatolewa kwa wahusika baada ya ukaguzi wa vitabu hivyo.

Kuhusu mitaro ya maji inayoharibu barabara za pembezoni mjumbe alitaka kujua hatua zilizochukuliwa. Ilifafanuliwa kuwa taarifa imetolewa TANROADS na Wizara husika hivyo utekelezaji unasubiri majibu yatakayopatikana. Aidha ilifafanuliwa kwamba barabara

ilijengwa kwa kufuata ramani iliyotolewa na kwamba madhara yaliyotokea baada ya ujenzi wa barabara yanapaswa kufidiwa na Serikali na si Kampuni iliyojenga.

Mjumbe mwingine alitaka kujua ni lini uwanja wa mpira unaanza kujengwa. Ilijibiwa kuwa fedha ya ujenzi huo ipo na kwamba taratibu za kutangaza zabuni zimeanza.

Kuhusu walengwa wa TASAF wasiokidhi vigezo walioondolewa kwenye malipo na kutakiwa kurejesha fedha, mjumbe alitaka kujua hatua iliyofikiwa baada ya walengwa hao kuomba rufaa. Ilifafanuliwa kuwa baada ya kukata rufaa walijaza fomu na zikapelekwa TASAF Makao Makuu na nakala ilipelekwa na Mhe. Mbunge kwa ajili ya ufuatiliaji.

Kuhusu ufanyikaji wa vikao vya kisheria kwa ngazi za Vijiji na Kata, wajumbe walisisitiza kwamba Vijiji na Kata wasiofanya vikao hivyo wasipatiwe ruzuku.

Taarifa zilipitishwa.

## **TAARIFA YA KAMATI YA ELIMU, AFYA NA MAJI**

Ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya Elimu, Afya na Maji kutokana na kikao kilichoketi tarehe 18/04/2017 kuanzia saa 4:09 asubuhi. Kikao hicho kilihudhuriwa na wajumbe 12 (kumi na mbili) kati ya 12 (kumi na mbili), Wataalam waliohudhuria walikuwa 20 (ishirini). Kikao kilizingatia agenda kama inavyooneshwa kwenye dondoo zifuatazo:

### **1.0 KUMB. NA. 11/2016/2017/03 - KUFUNGUA KIKAO.**

- 1.1 Akifungua kikao Mwenyekiti aliwakaribisha wajumbe katika kikao ili kujadili taarifa za utekelezaji robo ya tatu na aliwataka kuchangia kwa pamoja taarifa hizo.
- 1.2 Kikao kilifunguliwa mnamo saa 4:09 asubuhi.

### **2.0 KUMB. NA. 12/2016/2017/03 - KUTHIBITISHA DONDOO.**

- 2.1 Wajumbe waliridhia kuwa agenda zilizowasilishwa ndizo zijadiliwe.

### **3.0 KUMB. NA. 13/2016/2017/03 - KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 13/10/2016.**

- 3.1 Muhtasari ulisomwa na kufanya masahihisho yafuatayo
  - Uk 3. Neno “yalishaanza” lisomeke “walishaanza”
  - Uk 9. Neno “kilizimia” lisomeke “kiliazimia”
  - Uk 9. Neno “kweda” lisomeke “kwenda”
  - Uk 10. Neno “aisha” lisomeke “aidha”
  - Uk 11. Neno “utupati” lisomeke “utupaji”
- 3.2 Baada ya masahihisho hayo wajumbe waliridhia kuwa muhtasari huo usainiwe na kuwa kumbukumbu sahihi za kikao na kisha ulisainiwa na Mwenyekiti.

**4.0 KUMB. NA. 14/2016/2017/03 - TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 23/01/2017.**

- 4.1 **Hoja na 1:** Mjumbe mwingine alitaka kujua juu ya uhamasishaji kwa wananchi kujiunga na mfuko wa CHF kwamba ni viongozi wa ngazi ipi walioshirikishwa. Ilifafanuliwa kuwa walishirikishwa viongozi wa ngazi za Vijiji. **Liliwekwa Azimio** kuwa Mganga Mkuu wa Wilaya akutane na Viongozi wa kila Kata na Vijiji na Vitongoji kwa kuwakusanya katika Kata zao ili kufanya uhamasishaji kwao, wajiunge na mfuko wa CHF ili nao wakawahamasishe wananchi kufanya hivyo
- 4.2 **Utekelezaji** - Ilijibiwa kuwa Idara inaendelea kufanya uhamasishaji kwa njia ya Redio za kijamii na sherehe mbali mbali zinazojitokeza.
- 4.3 Wakijadili hoja hii wajumbe **waliazimia tena** kuwa azimio hilo litekelezwe upya kwa Mganga Mkuu wa Wilaya kukutana na Viongozi wa kila Kata na Vijiji na Vitongoji kwa kuwakusanya katika Kata zao ili kufanya uhamasishaji kwao, wajiunge na mfuko wa CHF ili nao wakawahamasishe wananchi kufanya hivyo.
- 4.4 **Hoja na 2** - Mjumbe alihoji ni mkakati gani umewekwa kwa Shule 10 duni za mwisho katika matokeo hayo. Ilifafanuliwa kuwa Mkurugenzi Mtendaji amekwisha agiza kuwa Shule 20 duni zifanyiwe ukaguzi haraka. Lilitolewa **azimio** kuwa Shule hizo zitambuliwe na mkakati wa namna ya kuzikwamua uwasilishwe. Aidha kwa Shule kumi bora za kwanza Walimu Wakuu wake waitwe katika kikao cha Baraza lijalo, wapongezwe, watangazwe kwenye vyombo vya habari na wapate chakula cha mchana na Waheshimiwa Madiwani na wapatiwe zawadi.
- 4.5 **Utekelezaji** - Mkakati wa kuzikwamua Shule kumi zilizofanya vibaya katika Mtihani wa Kumaliza Elimu ya Msingi mwaka 2016 uliambatishwa. Walimu Wakuu wa Shule zilizofanya vizuri (kumi bora kiwilaya) waliandikiwa barua za mwaliko wa kuhudhuria kikao cha Baraza la Madiwani.
- 4.5 Wajumbe walisisitiza kuwa katika kikao cha Madiwani cha robo ya tatu Walimu Wakuu wa Shule zilizofanya vizuri (kumi bora kiwilaya) waitwe bila kukosa.
- 4.6 **Hoja na 3** - Kuhusu uwasilishwaji wa taarifa ya utoro kwa wanafunzi, lilitolewa **Azimio** kuwa taarifa hiyo iwe inawasilishwa katika vikao hivi. Aidha taarifa hiyo ioneshwe pia hali ya nidhamu kwa walimu na hatua zilizochukuliwa.
- 4.7 **Utekelezaji** - Azimio lilizingatiwa na taarifa iliambatishwa.
- 4.8 **Hoja na 4** - Kuhusu taarifa za ukaguzi wa Shule, kikao **kiliazimia** kuwa taarifa hizo ziwe zinawasilishwa katika vikao vya Kamati.
- 4.8 **Utekelezaji** - Taarifa iliambatanishwa.
- 4.9 **Hoja na 5** - Kikao **kiliazimia** kuwa taarifa za mimba shuleni ziwe zinatolewa katika kikao.
- 4.10 **Utekelezaji** - Taarifa ilioneshwa kwenye taarifa ya Idara.
- 4.11 **Hoja na 6** - Kuhusu matukio ya wanafunzi wenye mimba Shule ya Sekondari Kiruruma, **iliagizwa** kuwa jambo hilo lifuatiliwe na taarifa itolewe.

- 4.12 **Utekelezaji** - Kesi ilifunguliwa Mahakamani mnamo tarehe 17/02/2017.
- 4.13 **Hoja na 7** - Kuhusu matukio yaliyopo ya wanafunzi wenye mimba shuleni kikao **kilizimia** kuwa matukio hayo yawasilishwe kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya ili kutoa msaada pale unapohitajika.
- 4.14 **Utekelezaji** - Taarifa ziliwasilishwa kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya kupitia kwa Mhe. Mkuu wa Wilaya.
- 4.15 **Hoja na 8** - Aidha ili kupunguza mimba shuleni kikao kiliweka mkakati na **kuagiza** kuwa Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wawezeshwe kwenda kutoa elimu mtambuka kwa wanafunzi ili wajitambue.
- 4.16 **Utekelezaji** - Agizo lilizingatiwa, Idara ya Maendeleo ya Jamii kwa kushirikiana na Idara za Elimu Msingi na Sekondari zilitoa mafunzo juu ya stadi za maisha kwa wanafunzi wa Shule za Sekondari Kayanga, Bugene, Ndama, Nyakasimbi, Kiruruma, Rwambaizi, Kituntu na Nyakahanga. Pia kupitia Redio za jamii elimu imekuwa ikitolewa kuhusu wanafunzi kujitambua na kufanya maamuzi sahihi.

## 5.0 **KUMB. NA. 15/2016/2017/03- TAARIFA ZA IDARA:**

### i. **IDARA YA AFYA.**

- 5.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika kwa kipindi cha robo ya tatu ikiwa ni pamoja na usimamizi wa watumishi, usimamizi wa fedha, usimamizi wa huduma za CHF, kusimamia huduma ya matibabu bure kwa wazee, kusimamia huduma za uzazi na mtoto, kudhibiti ugonjwa wa malaria kwa kufuatilia ubora wa upimaji wa ugonjwa wa malaria vituoni.
- 5.1 Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walieleza kuwa mfuko wa CHF bado haujahudumia vizuri wananchi kwani huduma zinatolewa kwa kusuasua na zoezi la kupiga picha na kupewa vitambulisho pia linachukua muda mrefu.
- 5.2 Ilifafanuliwa kuwa mikakati ya kurahisisha zoezi hilo inaendelea na kwamba hadi sasa jumla ya vituo nane vina kamera kwa ajili ya kupiga picha.
- 5.3 Wajumbe **waliazimia** kuwa taarifa kamili ya mfuko wa CHF kwa kila Kata iandaliwe, ikionesha mwenendo wa utoaji wa vitambulisho, utoaji wa huduma ikiwa ni pamoja na walengwa waliojiunga na mfuko huo kupitia mpango wa kunusuru kaya maskini - TASAF.
- 5.4 Kuhusu changamoto zinazokikumba Kituo cha Afya Kayanga zikiwemo upungufu wa vifaa tiba, madawa, vitanda, na miundombinu mbalimbali, wajumbe walishauri kuwa Kituo hicho kiborehwe na kuongezewa nguvu ili kiweze kutoa huduma bora kwa wananchi.
- 5.5 Wajumbe walishauri kuwa Idara ijitahidi kufanya usimamizi katika maeneo mbalimbali na kuhakikisha inapunguza vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano na mama wajawazito ikiwa ni pamoja na kuboresha huduma za mkoba kwa kuwasisitiza wananchi kujenga mabanda kwa ajili ya kutolea huduma.

- 5.6 Kuhusu watoa huduma za afya ngazi za vijiji, wajumbe walisisitiza kuwa Kamati za Maendeleo za Kata pamoja na Menejimenti waone namna ya kuwawezesha watu hao na **kuazimia** kuwa Idara ya Mipango itoe maelekezo kwa vijiji vyenye uwezo kuanza kuwalipa watoa huduma hao.
- 5.7 Kuhusu wagonjwa mbalimbali watakaonekana kuhitaji huduma ya gari la wagonjwa wajumbe **waliazimia** kuwa Mkuu wa Idara ya Afya awajulishe Waganga wa Vituo vya Afya pamoja na Zahanati kuratibu vizuri na kutoa taarifa mara moja pale unapohitajika msaada wa gari la wagonjwa kwa huduma za matibabu zaidi.
- 5.8 Ilitolewa hoja kuwa kuna baadhi ya wananchi wanaotolewa faini kinyume cha sheria kwa wasiokwenda kujifungulia Hospitalini. Iliazimiwa kuwa Idara ya Afya iandike barua kwa Watendaji wa Kata na nakala kwa Maafisa Tarafa kuwajulisha kuwa mwanachi asiyejifungulia Hospitali na asiyepeleka watoto kliniki waadhibiwe na Sheria mama kwa sasa, yaani kufikishwa kwenye Mabaraza ya Kijiji au Kata na sio kutozwa faini zisizo za kisheria.
- 5.9 Taarifa ya Hospitali ya Nyakahanga.**
- 5.10 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na huduma za kinga na tiba, huduma kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na kutoa huduma kwa wagonjwa wenye bima. Aidha taarifa ilionesha changamoto mbalimbali zinazojitokeza katika Hospitali ya Nyakahanga ikiwa ni pamoja na ongezeko la wagonjwa wanaohitaji msamaha, upungufu wa madawa na vifaa tiba, upungufu mkubwa wa watumishi, miundombinu chakavu na isiyotosha pamoja na uwepo wa vifaa chakavu.
- 5.11 Taarifa ilipitishwa.

## ii. IDARA YA MAENDELEO YA JAMII.

- 6.0** Taarifa iliwasilishwa ikionesha mikopo ya vikundi vya wanawake na vijana ambapo kwa robo ya tatu Januari - Machi jumla ya TSh. 8,000,000.00 zimetolewa kama mikopo kwa vikundi hivyo, ambapo kikundi kimoja ni wanawake na viwili ni vikundi vya vijana. Na fedha hizo zilitokana na mapato ya ndani. Aidha jumla ya TSh. 20,000,000.00 zilihamishwa kutoka mapato ya ndani kwenda mfuko wa wanawake na vijana ikiwa ni asilimia kumi kwa mwezi Januari - Machi 2017. Hata hivyo tangu mwaka wa fedha uanze 2016/2017 jumla ya TSh. 80,000,000.00 zimehamishwa kwenda mfuko wa wanawake na vijana.
- 6.1 Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walishauri kuwa Maafisa Maendeleo ya Jamii ngazi ya Kata wapewe taarifa pindi vikundi vyao vinapopewa mikopo ili waweze kufanya ufuatiliaji. Aidha waheshimiwa Madiwani wafanye ufuatiliaji wa vikundi vilivyopo kwenye maeneo yao kabla na baada ya kupewa mikopo.

- 6.2 Wajumbe **waliazimia** kuwa Idara ya maendeleo ya jamii iandae orodha ya vikundi vyote vilivyopewa mikopo na kuwapatia watendaji wa Kata na pia nakala wapewe Waheshimiwa Madiwani kwa ajili ya ufuatiliaji.
- 6.3 Taarifa ilipitishwa.

**i. IDARA YA ELIMU MSINGI.**

- 7.0 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika kwa robo ya tatu ikiwa ni pamoja na kuratibu na kusimamia zoezi la kuandikisha wanafunzi wa awali na darasa la kwanza 2017, kuratibu na kuendesha mafunzo kwa Kamati za Shule, kufanya ufuatiliaji wa ufundishaji shuleni na utekelezaji wa mpango wa kukuza stadi za kazi yaani KKK, kuratibu na kusimamia zoezi la usajili wa wanafunzi wote kuanzia darasa la kwanza hadi la saba kwenye mfumo maalum wa Baraza la Mitihani la Tanzania kwenye kumbukumbu za wanafunzi ujulikanao kama (Primary Record Management).
- 7.1 Wakijadili taarifa hii, wajumbe walitaka kujua ni kwanini taarifa ya utoro imezigusa shule kumi pekee. Ilifafanuliwa kuwa shule hizo ndizo zilizofanya vibaya zaidi kuliko nyingine lakini taarifa ya utoro kwa shule zote ipo.
- 7.2 Kuhusu upatikanaji wa Mratibu wa Elimu Kata Kata ya Ndama ilifafanuliwa kuwa suala hilo linashughulikiwa na ngazi ya Mkoa na tayari lipo kwenye utekelezaji.
- 7.3 Kuhusu changamoto zinazokikabili Kitengo cha Udhhibiti Ubora wa Shule wajumbe walishauri kuwa changamoto hizo ziainishwe na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi Mtendaji ili Wakaguzi waweze kuwezesha kufanya ukaguzi shuleni.
- 7.4 Taarifa ilipitishwa.

**ii. IDARA YA ELIMU SEKONDARI.**

- 8.0 Taarifa iliwasilishwa ikionesha mambo mbalimbali ikiwa ni pamoja na kusimamia mgao wa vitabu shuleni, kutembelea shule kupokea walimu wapya walioajiriwa na Serikali.
- 8.1 Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe **waliazimia** kuwa madeni mbalimbali yaliyotokana na ujenzi wa maabara yanayozikabili shule, suala hilo lirudishwe tena kwenye Baraza ili Baraza liamue nini kifanyike.
- 8.2 Kuhusu suala la utoro mashuleni wajumbe walishauri kuwa jambo hilo liwe ni ajenda ya kudumu katika vikao vyote vya kisheria ili kudumisha elimu.
- 8.3 Kuhusu wanafunzi wa kidato cha kwanza ambao hawajaripoti shuleni ushauri ulitolewa kuwa viongozi wa Kata na Vijiji washirikiane kusimamia kikamilifu suala hilo kwa kushirikiana na Waheshimiwa Madiwani kwa kutoa taarifa kamili za wanafunzi ambao hawajaripoti shuleni. Aidha kwa Kata zenye wanafunzi wengi ambao hawajaripoti, ulitolewa ushauri kuwa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya aombwe kutoa msisitizo wa Kiserikali zaidi.
- 8.4 Taarifa ilipitishwa.

### **iii. IDARA YA MAJI VIJIJINI**

**9.0** Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi mbalimbali zilizofanyika katika kipindi cha robo ya tatu ikiwa ni pamoja ukarabati wa Mradi wa Maji Kabindi Nyakaiga unaoendelea, utaratibu wa manunuzi wa kumpata mkandarasi wa kuchimba visima sita Omukakajinja na Chonyonyo unaendelea, kutoa elimu ya utunzaji wa vyanzo vya maji kwa kushirikiana na Afisa Mazingira na kufuatilia Mradi wa Maji Kibogoizi ambapo taratibu za kununua vifaa zinaendelea.

9.1 Wakijadili taarifa hiyo, mjumbe alitaka kujua ni lini Mradi wa Maji wa Chanika uliozinduliwa na Mhe. Mkuu wa Mkoa utanza kutoa huduma ya maji kwa wananchi. Ilifanuliwa kuwa mkandarasi yupo mbioni kuja kukamilisha Mradi huo.

9.2 Taarifa ilipitishwa.

### **iv. MAMLAKA YA MAJI MJINI.**

**10.0** Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi mbalimbali zilizofanyika katika kipindi cha robo ya tatu ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa maji ambapo jumla ya mita za ujazo 21,771 zilizozalishwa, kusafisha vyanzo vya maji, kufanya tathmini ya kazi za miradi ya maji kwa Omurushaka na Kayanga chini ya BUWASA, pamoja na marekebisho ya mitambo na mabomba ya maji.

10.1 Wakijadili taarifa hii mjumbe aliipongeza jitihada zinazofanywa na Serikali pamoja na wadau binafsi katika kutatua tatizo la upungufu wa maji Kata ya Kayanga.

10.2 Kuhusu watu binafsi wanaochimba maji wajumbe walitaka kujua kama watu hawa wamepatiwa vibali na kama uchimbaji huo hauwezi kuathiri vyanzo vingine vya maji. Ilifanuliwa kuwa vibali vya kuchimba maji vinatolewa Mkoani kabla ya kuanza kuchimba maji.

10.3 Wajumbe walishauri kuwa ufanyike ufuatiliaji na sheria iangaliwe upya kuhusu uchimbaji wa maji, wataalam wa maji wahusishwe ili kuhakikisha uchimbaji huo hauathiri vyanzo vya maji vinavyotumiwa na wananchi.

10.4 Kuhusu madeni mbalimbali ya maji wajumbe walitaka kujua mwenendo wa ulipaji wa madeni hayo, ambapo ilifanuliwa kuwa mwenye deni kubwa ni Taasisi ya Magereza wanaodaiwa 16,000,000.00 na kwamba wameanza kulipa, ambapo kwa mwezi wa tatu wamelipa jumla ya TSh. 2,500,000.00. wajumbe walisisitiza kuwa watu wote wasiolipa bili za maji wakatiwe huduma hiyo.

10.5 Taarifa ilipitishwa.

### **v. CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI (KDVTC).**

**11.0** Wakijadili taarifa iliyowasilishwa wajumbe walishauri kuwa kutokana na baadhi ya masomo kukosa wanafunzi wa kutosha, Mkuu wa Chuo aangalie namna ya kuunganisha

masomo kwa kuongeza masomo yenye tija kwa jamii kama vile ujasiriamali ili kuwavutia wanafunzi walio wengi. Aidha ilishauriwa kuboresha taaluma inayotolewa ili kuwasaidia wahitimu kujiunga na taaluma za juu.

11.1 Kuhusu ruzuku ya Chuo inayopaswa kutolewa na Halmashauri ilishauriwa kuwa Halmashauri iwe inatoa ruzuku hata kwa awamu ili kusaidia Chuo kujiendesha.

11.2 Taarifa ilipitishwa.

#### **vi. IDARA YA MAZINGIRA NA USIMAMIZI WA TAKA NGUMU.**

**12.0** Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na usimamizi wa usafi wa mazingira, usafi wa mitaa, uzoaji usafirishaji na utupaji wa taka ngumu, usimamizi wa hifadhi na utunzaji wa mazingira na usimamizi wa hifadhi ya mazingira (misitu na vyanzo vya maji).

12.1 Wakiijadili taarifa hiyo, wajumbe walieleza kuwa gari la taka halifiki baadhi ya maeneo na hivyo kuwa vigumu kuwachangisha wananchi ushuru wa taka. Ilifafanuliwa kuwa mkandarasi anayesafirisha taka amesaini mkataba mpya na kwamba atakuwa anafika maeneo mbalimbali ikiwemo Omugakorongo na Ndama.

12.2 Wajumbe walieleza kuwa Mradi wa Ujenzi wa barabara wa Kyaka – Bugene umesababisha athari nyingi za kimazingira kama uchafuzi wa vyanzo vya maji na kutiririsha maji kwenye makazi ya watu. Ilifafanuliwa kuwa tayari madhara yote yameainishwa, TANROADS Mkoa wamepewa taarifa na Afisa Mazingira anajiandaa kupeleka taarifa hiyo NEMC ili ufuatiliaji ufanyike mapema kabla mradi haujakabidhiwa kwa wananchi.

12.3 Kuhusu taarifa za upandaji wa miti zinazotolewa na Watendaji wa Kata wajumbe walishauri kuwa Afisa Mazingira alishauriwa kujiridhisha na taarifa hizo kwani nyingine huwa sio sahihi.

12.4 Ilitolewa taarifa kuwa wafugaji waliohamishwa kwenye pori la Kimisi na Burigi wamehamia Kata ya Nyakasimbi na kusababisha msongamano pamoja na magonjwa ya mifugo. Ilifafanuliwa kuwa viongozi wa Serikali ya Kijiji hawana mamlaka ya kuuza ardhi kwa wafugaji na kushauri kuwa Maafisa Tarafa wafuatilie na kujua uhalali wa ujio wa watu hao.

**12.5 Iliazimiwa** kuwa Afisa Mazingira na Idara ya Mifugo washirikiane ili kutatua tatizo hilo la uvamizi wa watu na mifugo katika Kata ya Nyakasimbi ambalo limesababisha mlipuko wa magonjwa ya mifugo.

12.6 Taarifa ilipitishwa.

#### **13.0 KUMB. NA. 16/2016/2017/03 - KUFUNGA KIKAO.**

13.1 Akifunga kikao Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa kuchangia kwa wakati taarifa zilizowasilishwa.

13.2 Kikao kilifungwa saa 9:00 alasiri.



Wakijadili taarifa hiyo mjumbe alihoji juu ya viwango vya faini kwa akina mama wasiojifungulia Hospitalini. Ilifafanuliwa kuwa adhabu zinatolewa za viwango tofauti tofauti kulingana na maeneo husika lengo ikiwa ni kuhamasisha akina mama kujifungulia Hospitalini.

Wajumbe walisitiza Idara ya Maendeleo ya Jamii kuendelea kutoa semina kwa Shule za Sekondari ili kuepuka mimba za utotoni. Aidha Idara iendelee kusimamia vikundi kurejesha fedha kwa wakati.

Mamlaka ya Maji Mjini ilishauriwa kuendelea kufuatilia madeni kwa wadaiwa wake hususani taasisi za Serikali kama Magereza ili kumalizia madeni.

Kuhusu uboreshaji wa huduma ya upimaji katika huduma ya Afya ilielezwa kuwa zimenunuliwa darubini 3 na kuna mpango wa kuongeza nyingine 4. Wajumbe walishauriwa kusimamia kwa karibu utoaji wa huduma za afua katika maeneo yao ikiwa ni pamoja na kujiridhisha na ubora wa huduma inayotolewa. Aidha wajumbe walishauriwa kuendelea kuhamasisha jamii kujiunga na CHF.

Kuhusu upelekaji wa ruzuku katika Chuo cha KDVTC wajumbe walishauri kwamba Chuo kendelee kutumiaa fedha zinazopatikana kwani kwa sasa Halmashauri haijapokea OC.

Taarifa ilipitishwa.

## TAARIFA YA UUM APRIL

Wakijadili taarifa hiyo mjumbe alitaka kujua kama kuna kifungu cha kurekebisha barabara zilizokatika. Ilijibiwa kwamba fedha hizo hazijaletwa hivyo viongozi washiriki kufanya uhamasishaji katika maeneo yao ili wananchi wafanye ukarabati katika maeneo yao.

Wajumbe walieleza kuwa barabara ya Nyakahanga - Nyabiyonza iliharibika sana na kushauri kwamba marekebicho yake yafanyike kwa wakati.

Kuhusu vikundi vilivyopokea mizinga wajumbe walishauri mtaalam wa nyuki kutembelea vikundi hivyo, kukagua mizinga na kutoa ushauri wa kitaalam.

Kuhusu magonjwa ya mifugo wajumbe walishauri kuwa utaratibu wa chanjo za mifugo ufanyike haraka ili kuhakikisha mifugo yote inapewa chanjo. Aidha wajumbe **waliazimia** kuwa ifanyike sensa ya mifugo ili kutambua idadi kamili ya mifugo na kwamba chanjo zitolewe kulingana na idadi hiyo.

Kuhusu ushuru wa samaki, wajumbe walisisitiza kuwa ushuru huo ulipiwe maeneo ya mwaloni na kwamba atakayebainika hajalipia ushuru huo achukuliwe hatua za kisheria.

Wajumbe walitahadharisha juu ya uvamizi wa ardhi baada ya wafugaji kuondolewa katika pori la Kimisi na kushauri kuwa maeneo yote yasimamiwe na kuchukuliwa hatua kwa atakayebainika kuvamia.

Taarifa ilipitishwa.

### **TAARIFA YA KAMATI KUDHIBITI UKIMWI.**

Ifuatayo ni taarifa ya Kamati ya kudhibiti UKIMWI kutokana na kikao kilichoketi tarehe 24/04/2017 kuanzia saa 4:45 asubuhi. Kikao hicho kilihudhuriwa na wajumbe 6 kati ya 6, wajumbe waalikwa 08 na wataalam 10. Kikao kilizingatia agenda kama zinavyoonesha kwenye dondoo zifuatazo;

#### **1.0 KUMB. NA. 14/2016/17- KUSOMA NA KUTHIBITISHA MUHTASARI WA KIKAO CHA TAREHE 18/01/2017.**

1.1 Wajumbe waliusoma muhtasari na kuridhia kuwa uwe kumbukumbu sahihi za kikao na kisha ulisainiwa na Mwenyekiti.

#### **2.0 KUMB. NA. 15/2016/17- TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA KIKAO CHA TAREHE 18/01/2017.**

2.1 **Hoja na 1** - Wajumbe walijadili na **kuazimia** kuwa sheria hiyo inayofafanua na kuruhusu au kuzuia mikesha ipelekwe ngazi za kata na vijiji ili iweze kueleweka na kusimamiwa kuanzia ngazi za chini.

2.2 **Utekelezaji** - Sheria Na. 28 ya mwaka 1968 kifungu cha 14(1)-(3) ilitumwa kwa Watendaji wote wa Kata na Vijiji kwa barua yenye kumb. Na. AF.20/118/01/44 ya tarehe 27/01/2017.

2.3 **Hoja na 2** - Liliwekwa **azimio** kuwa shirika lolote linalokuja au linaloanzishwa ili kutoa huduma kwa WAVIU lazima lianzie Idara ya Maendeleo ya Jamii ili kutambuliwa.

2.4 **Utekelezaji** - Azimio lilizingatiwa.

#### **3.0 KUMB. NA. 16/2016/17- TAARIFA ZA UTEKELEZAJI.**

i. **Mradi wa kudhibiti UKIMWI wa Halmashauri ya Wilaya.**

4.0 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa elimu juu ya sheria ya kudhibiti na kupambana na VVU na UKIMWI, kushiriki zoezi la kupiga picha walengwa linaloendelea, ugawaji wa vyakula vya lishe kwa watoto waishio na VVU na uhamasishaji upimaji wa VVU kwa hiari.

- 4.1 Wakijadili taarifa hii, wajumbe waliazimia kuwa Mratibu wa UKIMWI aboreshe taarifa yake kwa kutoa taarifa yenye takwimu mbalimbali.
- 4.2 Kuhusu uendeshwaji wa Kamati za Kudhibiti UKIMWI ngazi ya Kata wajumbe walitaka kujua mpango wa Idara kutaka kuziwezesha kupata posho. Ilifafanuliwa kuwa Kamati hizo zinatakiwa kukaa kama zinavyokaa kamati nyingine za ngazi ya Kata na Vijiji. Wajumbe walishauri kuwa Halmashauri iwasiliane na Serikali ngazi za juu kuona namna ya utatuzi wa jambo hilo.
- 4.3 Aidha ilishauriwa kuwa ajenda ya UKIMWI iwe ya kudumu katika vikao vyote vya WDC ili kupunguza gharama za uendeshaji wa vikao.
- 4.4 Kuhusu kupokea fedha za msaada kutoka kwa wadau mbalimbali mjumbe alihoji kuwa kuna baadhi ya walimu wakuu wanaokataa kupokea fedha hizo kutokana na sera ya Elimu Bure, ilifafanuliwa kuwa Waraka upo wazi na unafafanua vizuri kuhusu baadhi ya michango na huduma mbalimbali ambazo wazazi au wahisani mbalimbali wanatakiwa kuhudumia watoto.
- 4.5 Wajumbe **waliazimia** kuwa Waraka huo wa sera ya Elimu Bure usambazwe kwa wadau mbalimbali wakiwemo Mashirika yasiyo ya Kiserikali ili kupata uelewa wa pamoja.
- 4.6 Taarifa ilipitishwa.

**ii. Ofisi ya Mganga Mkuu.**

- 5.0 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika zikiwemo, kupima VVU kwa kushirikiana na AMREF ambapo Kata nane za Kiruruma, Kibondo, Bweranyange, Igurwa, Chonyonyo, Ihembe, Nyabiyonza na Rugu ambapo jumla ya wananchi 3,738 walijitokeza kupima afya zao na kati ya hao 24 waligundulika kuwa na maambukizi na kufanya tohara ambapo wanaume 21,777 walijitokeza ambao ni sawa asilimia 156.
- 5.1 Wakijadili taarifa hii, wajumbe waliazimia kuwa taarifa kamili ya watu waliopima VVU iandaliwe na kuwasilishwa kikao kijacho.
- 5.2 Taarifa ilipitishwa.

**iii. Ustawi wa Jamii.**

- 6.0 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa huduma kwa familia na watoto wenye mazingira magumu ambapo ofisi imeendelea kupokea migogoro yote ihusuyo ndoa, matunzo, utelekezaji wa watoto na familia, huduma kwa Wazee ambapo jumla ya wazee 12,498 wameshapata vitambulisho vya matibabu na utambuzi unaendelea kwani wazee huongezeka kila siku.
- 6.1 Wakijadili taarifa hii, wajumbe walishauri kuwa Kitengo cha Ustawi wa Jamii kiwezeshe kutekeleza shughuli zao kwa kushirikiana na Idara ya Maendeleo ya Jamii na Idara ya Afya.

- 6.2 Wajumbe walishauri kuwa taarifa iwe inaonesha idadi ya watu waliopata rufaa kutoka Hospitalini kwenda Kitengo cha Ustawi wa Jamii. Aidha Afisa Ustawi wa jamii aelekeze watu namna ya kupata huduma ya utatuzi wa migogoro katika Jamii, pia afanye ziara vijijini kutoa huduma kwa wananchi.
- 6.3 Taarifa ilipitishwa.

**iv. Mwakilishi wa Asasi za Kiraia.**

➤ **WOMEDA**

- 7.0 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kuzuia mimba mashuleni, kuzuia ndoa za utotoni, kutoa elimu ya jinsia na afya za uzazi na kutoa elimu ya kuzuia VVU na UKIMWI. Vijana walioshiriki kupata Elimu katika Shule nne ni 1,530 wavulana 612 na wasichana 918. Shule za Sekondari zilizopata huduma hiyo ni Kihanga, Ndama, Kituntu na Rwambaizi.

➤ **KVTC**

- 7.1 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya maadili na magonjwa yatokanayo na kujamiiana kwa vijana wa shuleni na vyuoni, kufadhili na kutoa mafunzo kwa vijana yatima na wanaoishi katika mazingira magumu, kutembelea na kutoa elimu rika katika Vijiji vitano ambavyo ni Ndama, Lukaka, Kakiro, Runyaga na Chanika.

➤ **ACP/ELCT KARAGWE**

- 7.2 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kupokea ripoti za maendeleo ya wanafunzi na kutoa barua za ahadi kulingana na makubaliano, kukamilisha ripoti ya mwaka 2016 na kuituma kwa wafadhili, kufanya vikao vya wahisani kuhusu shughuli za miradi.

➤ **TUMAINI FUND**

- 7.3 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa huduma ya pesa taslimu kila mwezi TSh. 5,000/- kwa kila mtoto yatima kwa familia 42, kugawa vifaa mbalimbali kama nguo, vyandarua, daftari, sare za shule na kalamu kwa familia 129 zilizosajiliwa zenye watoto yatima 236, kugawa mahindi kilo 756 katika Shule ya Msingi Suzana, na kilo 540 Shule ya Msingi Maguge.

➤ **KAKAYODA**

- 7.4 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa elimu ya kudhibiti maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI kupitia mikutano ya hadhara, kutoa elimu ya siku tatu ya kujiepusha na ndoa za utotoni kwa wasichana wanaojifunza ufundi cherehani.

➤ **SODIT BUGENE**

- 7.5 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa watu 11 juu ya athari za matumizi ya sabuni na vipodozi viambatasumu, mafunzo ya kutengeneza sabuni na mafuta kwa kutumia miti asilia na kutoa ushauri nasaha kwa WAVIU.

➤ **BCPA**

- 7.6 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na ugawaji wa kondom za kiume katika nyumba za kulala wageni Nyakaiga, kufanya mikutano mbalimbali.

➤ **SAWAKA**

- 7.7 Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kutoa huduma mbalimbali zinazohusiana na VVU na UKIMWI kwa wazee, watoto yatima walioko katika mazingira hatarishi, WAVIU, wajane na watu wenye ulemavu.

- 7.8 Wakijadili taarifa hizo. Mjumbe alitaka kujua mchango wa ASASI kwa jamii katika kukabiliana na kesi zinazokuwepo mahakamani. Ilifafanuliwa kuwa kazi ya ASASI ni kusuluhisha na kutatua migogoro, lakini wao sio mawakili kwa kuwasaidia wananchi kuendesha kesi mahakamani kwa hivyo mwananchi hutakiwa kujisimamia mwenyewe mahakamani au kutafuta wakili.

**v. Viongozi wa Madhehebu.**

**a. Ki-Kikristo**

- 8.0 Taarifa iliwasilishwa na wajumbe walishauri kuwa madhehebu ya dini kwa kushirikiana na Idara za Elimu wajitahidi kuendelea kutoa elimu juu ya VVU na UKIMWI kwa wanafunzi hasa pale yanapotokea makusanyiko mbalimbali ya kidini au kishule yanayowahusisha wanafunzi.

- 8.1 Taarifa iliwasilishwa.

## **vi. Mwakilishi wa NACOPHA.**

**9.0** Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kushiriki zoezi la upimaji wa hiari linaloendelea, kushawishi wadau kujenga uwezo katika masuala mbalimbali yahasuyo UKIMWI, kuelimisha jamii kuwa wazi kuhusu VVU na UKIMWI, kuhamasisha wanachama kujiwekea hisa kwenye vikundi ili kukabiliana na changamoto ya kukosa mtaji katika vikundi. Aidha taarifa ilionesha mafanikio yaliyopatikana ikiwa ni pamoja na kupata vyakula kwa watoto waishio na VVU kupitia vikundi vya CTC.

9.1 Taarifa ilipitishwa.

## **vii. Mwakilishi wa Vijana.**

**10.0** Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kusaidia wanawake na vijana kupata uwezeshwaji, kusaidia vijana kupata elimu juu ya ushirika, kutoa elimu juu ya athari za UKIMWI kwa vijana.

10.1 Wakijadili taarifa hiyo wajumbe walishauri kuwa vijana wanaopewa mikopo wapatiwe na ushauri juu ya biashara za kufanya ili kuweza kurejesha mikopo hiyo ili kuepuka kuwapeleka mahakamani wanaoshindwa kurejesha mikopo kwa muda unaotakiwa.

10.2 Kuhusu msisitizo juu ya matumizi ya dawa za kupunguza makali ya VVU na UKIMWI wajumbe walishauri kuwa jamii ipewe elimu ya kutosha ili iendelee kutumia dawa hizo na kwamba wasichanganye imani za dini zao na matumizi sahihi ya dawa hizo.

10.3 Wajumbe walisisitiza kuwa Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ataarifiwe kuwaelimisha baadhi ya viongozi wa madhehebu ya dini kutowapotosha wananchi juu ya matumizi sahihi ya dawa za kupunguza makali ya UKIMWI.

10.4 Kuhusu taarifa za ASASI na wadau mbalimbali katika kikao hiki, wajumbe **waliazimia** kuwa Idara ya Maendeleo ya Jamii na Idara ya Afya ziwe zinafanya uchambuzi wa masuala yaliyowasilishwa ikiwa ni pamoja na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa kazi zao, ili kuona namna ya utatuzi na utekelezaji wa masuala hayo yanayojitokeza.

## **viii. Taarifa ya Afisa Utamaduni.**

**11.0** Taarifa iliwasilishwa ikionesha kazi zilizofanyika ikiwa ni pamoja na kufanyika kwa michezo ya kirafiki ya mpira wa miguu, maadhimisho ya siku ya wanawake duniani tarehe 8/3/2017 na kushiriki maadhimisho ya siku ya maji duniani, yaliyofanyika kimkoa wilayani Karagwe.

- 11.1 Wakijadili taarifa hii wajumbe walishauri kuwa wanamichezo wapewe elimu juu ya VVU na UKIMWI kila baada ya mechi kwisha. Aidha Afisa Utamaduni arekebishe baadhi ya sentensi/kauli zinazotumika kwenye taarifa zake.
- 11.2 Taarifa ilipitishwa.

**12.0 KUMB. NA. 16/2016/17- KUFUNGA KIKAO.**

- 12.1 Akifunga kikao Mwenyekiti aliwapongeza wajumbe kwa mawazo na michango yao makini.
- 12.2 Kikao kilifungwa mnamo saa 8:48 mchana.

Wakijadili taarifa hiyo, wajumbe walishauri kuwa suala la udhibiti UKIMWI liendelee kwa ushirikiano wa viongozi na wanachi wote.

Taarifa ilipitishwa.

**KUMB NA 98/2016/2017/8 - TAARIFA ZA MKURUGENZI MTENDAJI.**

**I. TAARIFA YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWEZI MACHI 2017.**

Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri ilikisia kukusanya na kutumia kiasi cha fedha chenye jumla ya TSh. 34,771,925,911.65 hata hivyo kwa mwezi Machi 2017 Halmashauri ya Wilaya imekusanya kiasi cha TSh. 2,659,526,013.23 ambapo jumla ya mapato Julai 2016 hadi mwezi Machi 2017 ni jumla ya TSh. 23,376,065,020.34 ambayo ni sawa na 67.23%.

Kwa upande wa matumizi kwa mwezi Machi 2017 Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe imetumia jumla ya TSh. 2,837,318,827.13 ambapo jumla ya matumizi kwa mwezi Julai 2016 hadi mwezi Machi 2017 ni TSh. 24,216,773,540.69 ambayo ni sawa na 64.77% ya lengo kwa mwaka.

Wakijadili taarifa hiyo wajumbe walishauri kwamba mkakati wa kukaza hukumu uendelee na ukamilishwe ili Halmashauri iweze kulipwa kwa kesi ilizoshinda.

Kuhusu ukusanyaji wa mapato ngazi ya Kata, Wah. Madiwani walishauriwa kuwaelekeza Watendaji wa Kata kutoa taarifa sahihi za mapato kupitia vikao vya WDC.

Kuhusu usahihi wa mapato kutoka vyanzo mbalimbali wajumbe walishauri kwamba Mkuu wa Idara ya Fedha na Biashara na Mkuu wa Kitengo cha TEHAMA wafanye marekebisho kwenye mfumo ili kuhakikisha mapato yanaendana na vyanzo vyake.

Wajumbe waliishauri Menejimenti kujitahidi kuziba mianya yote ya upoteaji wa mapato ikiwa ni pamoja na kuboresha mazingira ya wakusanyaji wa mapato.

Taarifa ilipitishwa.

**II. TAARIFA YA MANUNUZI NA BODI YA ZABUNI KWA KIPINDI CHA JANUARI - MACHI, 2017.**

Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri ilikisia kununua vifaa, kazi na huduma mbalimbali vyenye thamani ya TSh. 5,181,938,618.70 kwa mwaka. Ambapo kwa mwezi Machi 2017 Halmashauri ilikisia kufanya manunuzi ya TSh. 431,828,212.23 ambapo manunuzi halisi yaliyofanyika ni yenye thamani ya TSh. 154,224,822.59 ambayo ni sawa na asilimia 35.7.

Kwa robo ya tatu Halmashauri ilikisia kununua vifaa/huduma mbalimbali vyenye thamani ya TSh. 1,295,484,654.69 ambapo manunuzi ya kawaida yaliyofanyika ni yenye thamani ya TSh. 320,173,149.47 ambayo ni sawa na asilimia 24.7.

Taarifa ilipitishwa.

**III. TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI JULAI- MACHI, 2017.**

Taarifa iliwasilishwa kuwa kwa mwaka wa fedha 2016/17 Halmashauri imeidhinishiwa kiasi cha TSh. 5,643,393,738.61 ili kutekeleza na kusimamia miradi ya maendeleo.

Kwa kipindi cha Julai - Machi 2016/17 Halmashauri ilipokea fedha kiasi cha TSh. 6,060,488,172.67 kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Ambapo katika fedha hizo kiasi cha TSh. 1,413,011,969.54 ni bakaa ya mwaka 2015/16 na TSh. 4,647,476,204.13 zimepokelewa katika kipindi cha Julai - Machi 2017 sawa na asilimia 82.4 ya makisio kwa mwaka wa fedha 2016/17.

Taarifa ilipitishwa.

**IV. TAARIFA YA MIKOPO YA VIKUNDI VYA WANAWAKE NA VIJANA KWA ROBO YA TATU, 2016/2017.**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha mikopo ya vikundi vya wanawake na vijana ambapo kwa robo ya tatu Januari - Machi jumla ya TSh. 8,000,000.00 zimetolewa kama mikopo kwa vikundi hivyo, ambapo kikundi kimoja ni wanawake na viwili ni vikundi vya vijana. Na fedha hizo zilitokana na mapato ya ndani. Aidha jumla ya TSh. 20,000,000.00 zilihamishwa kutoka mapato ya ndani kwenda mfuko wa wanawake na vijana ikiwa ni asilimia kumi kwa mwezi Januari - Machi 2017. Hata hivyo tangu mwaka wa fedha



uanze 2016/17 jumla ya TSh. 80,000,000.00 zimehamishwa kwenda mfuko wa wanawake na vijana.

Wakiijadili taarifa hiyo wajumbe walisisitiza kuwa taarifaya vikundi vilivyokopeshwa iwe inatolewa kwa Watendaji wa Kata na Wah. Madiwani.

Taarifa ilipitishwa.

**V. TAARIFA YA VIKAO VYA KISHERIA VILIVYOFANYIKA NGAZI YA KATA NA VIJJI KWA ROBO YA TATU 2016/2017.**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha vikao vya kisheria vilivyofanyika kwa robo ya tatu ngazi ya Kata na Vijiji na watumishi walioondolewa kwenye orodha ya malipo ya mishahara na taarifa ya upimaji wa wazi wa utendaji kazi (OPRAS).

Taarifa ilipitishwa.

**VI. TAARIFA YA UKAGUZI WA NDANI KWA KIPINDI CHA ROBO YA TATU, 2016/2017**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha jumla ya hoja 14, ambapo hoja nne zilikuwa ni za kipindi cha nyuma na 10 za robo ya tatu.

Wakiijadili taarifa hiyo wajumbe walishauri kuwa Menejimenti iandae majibu ya hoja kwa usahihi na kwamba ukaguzi unapofanyika ngazi za Vijiji na Kata mrejesho utolewe kwa wahusika.

Aidha wajumbe walisisitiza kuwa wakandarasi wanaopata kazi ngazi za Kata waelekezwe kutumia mashine za EFD ili kuondoa hoja za ukaguzi.

Wajumbe **waliazimia** kuwa mwongozo utolewe na Halmashauri kwa barua kuelekeza Taasisi zote kufanya manunuzi kwa watu wenye mashine za EFD.

Taarifa ilipitishwa.

**VII. TAARIFA YA MADENI YA UJENZI WA VYUMBA VYA MAABARA SHULE ZA SEKONDARI.**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha jumla ya TSh. 121,795,680.00 ambazo wanadai wazabuni mbalimbali waliotoa huduma kwa ajili ya ujenzi wa maabara katika Shule mbalimbali za Sekondari.

Wakiijadili taarifa hiyo wajumbe walikubaliana kwamba kila Kata ipelekewe madeni yake na kuhakikisha mkakati wa ulipaji wa madeni hayo unafanyika kupitia WDC.

Taarifa ilipitishwa.

## **VIII. MAPENDEKEZO YA KUREKEBISHA SHERIA NDOGO NA. 01 VIPENGELE 1-9 YA MWAKA 2011, JUU YA KODI ZA USOMBAJI WA MADINI YA UJENZI.**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha sheria iliyopendekezwa kubadilishwa na kwamba katika sheria ndogo hiyo utumikaji wake ulikua na ufanisi mdogo. Aidha sheria hiyo ilitungwa ikilenga kukusanya kodi/ushuru kwa kutumia vizuizi vya barabarani yaani “barrier”.

Kutokana na madini kusafirishwa kwa kupitia barabara nyingi za mtaani ni dhahiri kuwa ‘barrier’ hizo zilizoko barabara kuu zilikusanya kwa kiasi kidogo tu ushuru huo. Vilevile upo usombaji wa madini unaoishia kabla ya kufikia ‘barrier’. Pia baadhi ya madereva wamebainika wakisomba madini siku za mwisho wa wiki na pia siku za wiki kuanzia saa moja usiku.

Kutokana na hali hiyo, hali halisi ya ukusanyaji wa ushuru huo kwa sasa haijafikia asilimia 50, hivyo Timu ya Menejimenti ya Mamlaka ya Mji Mdogo inatoa ushauri wa kufanya mabadiliko ya sheria hiyo ili kuona kama chanzo hicho kinaweza kuwa na uhakika katika ukusanyaji kama ilivyoshauriwa na Mwanasheria wa Halmashauri

Wakiijadili taarifa hiyo wajumbe waliridhia kuwa mabadiliko hayo yafanyike haraka kwa kufuata taratibu zinazotakiwa, ili ianze kutumika kwa mwaka wa fedha 2017/2018 kwa lengo la kuongeza mapato ya Halmashauri.

Taarifa ilipitishwa.

## **IX. MAPENDEKEZO YA WAJUMBE WA BARAZA LA KATA BWERANYANGE.**

Taarifa iliwasilishwa ikionesha mapendekezo ya wajumbe wapya wa Baraza la Kata ya Bweranyange kama ifuatavyo;

- |                          |            |
|--------------------------|------------|
| 1. Hussein M. Kashangaki | Mwenyekiti |
| 2. Stewart Nicholas      | Katibu     |
| 3. Adrian M. Domisian    | Mjumbe     |
| 4. Najib H. Katuku       | Mjumbe     |
| 5. Abdul Bagoka          | Mjumbe     |
| 6. Retisia Dionizi       | Mjumbe     |
| 7. Rozimel M. Pastory    | Mjumbe     |
| 8. Marius A. Bwenge      | Mjumbe     |

Wakiijadili taarifa hiyo wajumbe walipitisha majina hayo kwa kuwa yalikiidhi vigezo vya kisheria.

Taarifa ilipitishwa.

**KUMB. NA. 99/2016/2017/8 - KUFUNGA KIKAO.**

Akifunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa mawazo yao na hivyo kufanikisha kikao. Alisisitiza Halmashauri kuendelea kukusanya mapato kikamilifu ili kufikia malengo ya Serikali ya kukusanya asilima 80. Alitoa wito wa kuwezesha kwa baadhi ya Idara zinazowafikia wananchi moja kwa moja mfano Idara ya Kilimo na Mazingira ili kuwafikia wananchi na kuwapatia elimu kwa masuala ya kilimo, uhifandhi wa mazingira na kutochoma moto ovyo.

Kuhusu dodoso linaloandaa taarifa za Kata alieleza kuwa dodoso hilo liboreshwe kwa kuongezea vipengele muhimu ili kuboresha taarifa hizo. Aidha Kamati za UKIMWI na Kamati za Maendeleo za Kata ziendeleo kufanya vikao vyake vya kisheria kikamilifu na kuwasilisha mihtasari yake kwa ngazi husika.

Alieleza kuwa Idara ya Ardhi iendeleo kufanya uhamasishaji kwa wananchi kupima maeneo yao kupitia makampuni binafsi yanayoendelea kufanya upimaji huo katika maeneo mbalimbali.

Alisisitiza kuwa suala la mifugo iliyohamishwa kutoka pori la Kimisi iendeleo kudhibitiwa kwa kutambuliwa rasmi. Aidha alitoa wito kwa Kamati ya Ulinzi na Usalama kuendelea kudhibiti suala la wahamiaji haramu na wahamiaji holela ndani ya Wilaya.

Kikao kilifungwa mnamo saa 11:26 jioni.

Wolta Kirita  
**KATIBU**

Wallace Mashanda  
**MWENYEKITI**

**Umethibitishwa leo.....**